SUPA JACKPOT
TZS. 1,154,861,566
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

# Nipashe

Alhamisi Septemba 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581440
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 2

**Samia** aagiza kukomeshwa usafi shambani kwa moto



UKURASA WA 9

**Mahakama** Kuu yasema tangazo la waziri ni batili mgogoro Loliondo



UKURASA WA 19

**Kagame:** Magharibi mnisamehe, nitawania tena urais mwakani



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa

UMEME WA RATIBA

# Vigogo wajifungia siku 3 kusaka suluhu

• **Waziri** Mkuu aorodhesha mikakati Tanzania kung'ara uzalishaji nishati hiyo... *Ukurasa wa 3*



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko




Sehemu ya washiriki wa Jukwaa la Nishati lililozinduliwa katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam jana.

## Watoa angalizo mkataba mpya Bandari bei za bidhaa

UKURASA 5

Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Mbarali, Missana Kwangura (kushoto), akikabidhi cheti kwa mshindi wa uchaguzi mdogo wa ubunge wa jimbo hilo, Bahati Ndingo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), baada ya kumtangaza wilayani Mbarali jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



# CCM yashinda Mbarali, waliopiga kura theluthi

• **ACT** yalalamika rafu vituoni, mawakala; yaambulia kura 18%... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** SIMBA SC YAITISHA COASTAL UNION UK.24 **KATUNI** UK.6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Meneja Mwandamizi Idara ya Wateja Wakubwa upande wa Nishati wa Benki ya NMB, Hamis Njapuka (kulia), kuhusu utayari wa benki hiyo katika maendeleo ya nishati, wakati wa kongamano la kimataifa la nishati, jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia aonya usafi mashambani kwa moto

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan amewaonya wananchi wa mkoa wa Lindi, kutumia moto wanaposafisha mashamba, badala yake watumie majembe na zana zingine kuepusha uharibifu wa mazao na mazingira.

Pia amewaelekeza viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, kutumia fedha zitakazopatikana katika kiwanda cha kutengeneza vioo cha 'sapphire' kuleta maendeleo ya wananchi badala ya kujiongezea fedha za posho za vikao.

Sambamba na hayo, amesema serikali iko mbioni kwa kuweka skimu ya umwagiliaji katika bonde la Mto Rufiji ili kuongeza uzalishaji zao mpunga kwa ajili ya kuinua maisha ya wakulima wa zao hilo na uchumi wa taifa.

Rais Samia aliyasema hayo jana kwa nyakati tofauti alipozungumza na wananchi wakati akitokea mkoani Lindi kwenda Dar es Salaam na kufungua kiwanda cha kisasa cha kutengeneza vioo cha 'sapphire' katika Kijiji cha Mkiu wilayani Mkuranga.

Alisema kusafisha mashamba kwa kutumia moto kuna athari nyingi, zikiwamo kupunguza uwezo wa mikorosho kuzaliana kwa wingi, kuharibu mazingira ya miundombinu na nguzo za umeme.

"Ndugu zangu mnapotumia moto husambaa kwenda kudaka na kuunguza miti ya mikorosho na nguzo za umeme na kusababisha hasara kwa jamii na shirika," alisema Rais Samia.

Rais aliwaagiza viongozi wa ngazi za mkoa na wilaya kusimamia shughuli hizo ili kudhibiti wakulima wachoma moto kwa kuwa wakiendelea kufanya hivyo, watasababisha hasara kwa maeneo mengi ya kiutawala zikiwamo taasisi na jamii.

Kuhusu skimu ya umwagiliaji kwa wananakijiji wa Ikwiriri, Rais alisema ujenzi utaanza mwaka huu kwa bwawa lenye ukubwa wa hekta 3,000 katika sehemu ya bonde hilo lenye kilometa 60 na litaendelea kuongezwa kila mwaka mpaka litakapokamilika.

Alisema lengo la ujenzi huo ni kuwawezesha wakulima kuzalisha mpunga kwa kuwa ni moja kati ya mazao yanayoelekea kuwa na soko kubwa kimataifa.

"Kwa hiyo na mpunga nao ni biashara kubwa. Tanzania tunauza mpunga Ulaya sasa hivi. Kwa hiyo niwaombe sana tunakuja kujenga skimu za umwagiliaji, naomba sana ingieni hasa vijana," alisema.

Aliwasisitiza vijana kujiunga katika mradi wa jenga kesho iliyo bora (BBT) ambao katika mkoa huo utajikita kutoa mafunzo ya kilimo cha mpunga lengo likiwa kuwakomboa vijana kupitia zao hilo.

Rais aliupongeza uongozi wa mkoa wa Pwani kwa kuweka mazingira ya uwekezaji na kuwasisitiza viongozi wa halmashauri hiyo kuweka mbele maslahi ya wananchi katika fedha zitakazopatikana kupitia uwekezaji huo.

Aliwaelekeza wananchi wanaoishi maeneo ambayo malighafi za kutengenezea vioo hivyo zitachimbwa kuweka kuzingatia uhifadhi wa mazingira yao ili yawe katika hali nzuri.

Serikali, alisema inaendelea kuweka mazingira bora ya uwekezaji ambapo mwaka jana ilitunga sheria mpya ya uwekezaji ambayo kwa kiasi kikubwa imetatua changamoto za kiuwekezaji ikiwamo utoaji wa vivutio kwa wawekezaji wa kimkakati.

"Pia sheria hii mpya imeweka mkazo katika kuwawezesha wawekezaji wa ndani na tukafanya marekebisho ya sheria ya ajira za wageni ambayo imetatua changamoto ya muda mrefu ya upatikanaji wa vibali vya kazi na ukaazi kwa wafanyakazi wageni," alisema Rais.

Aliwakumbusha pia wawekezaji kuteketeza takwa la kisheria ya ajira na mahusiano kazini la mpango wa urithishwaji wa ujuzi wa wazawa, ili kuwapa ujuzi na kuwapunguzia gharama za kuajiri wataalamu kutoka nje ya nchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema kupitia kiwanda hicho, serikali inatarajia kupata mapato mapya ya kodi ya Sh. bilioni 42.79 kwa mwaka.

Pia alisema mradi huo utaiingizia serikali dola za kimarekani milioni 164.8 na kuokoa dola za kimarekani milioni 54.75 ambazo zimekuwa zikitumika kununua bidhaa zinazozalishwa katika kiwanda hicho.

"Mpaka jana (juzi) kiwanda hiki kimeshaajiri watu 750. Kati ya hao asilimia 49 ni mafundi mchundo na watendaji na asilimia 39 ni mafundi wasiohitaji ujuzi maalum. Wahandisi wenye shahada ni watano pekee, maofisa rasilimali watu ni 12, wahasibu mauzo 12 na huduma kwa wateja ni asilimia moja," alisema.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema asilimia 80 ya malighafi zinazotumika katika kiwanda hicho zitatoka ndani, hivyo kuiongezea nchi fedha za kigeni na kuinua uchumi.

Pia alisema asilimia 20 ya malighafi ambazo kiwanda hicho kinaagiza nje ni madini ya 'soda ash' na chuma ambaye yanapatikana katika Engaruka na kuiomba serikali iwaboreshee miundombinu ya eneo hilo ikiwamo barabara, umeme na maji ili mwekezaji achimbe madini hayo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambaye pia ni Mbunge wa Mkuranga, Abdallah Ulega, alimwomba rais kuharakisha uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam, ili kuwapunguzia gharama wawekezaji wanaotumia bandari hiyo na kuwavutia wengi.

"Mazungumzo tukifanya na wawekezaji hawa wanachonilalamikia wanasema wanatumia gharama kubwa sana pale bandarini. Wananilalamikia kuwa kwa siku moja wanatozwa Dola 1000 (Sh.2,550,000)," alisema.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Frank Yang, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji hali ambayo itachangia kukua kwa uchumi wa nchi.

Alisema mradi huo ulioanza mwaka 2020, una thamani ya dola milioni 331 sawa na Sh. bilioni 745.7 na unatarajia kutoa zaidi ya ajira 1,650 kwa Watanzania, hivyo kupunguza tatizo hilo kwa vijana.

# CCM yashinda Mbarali, waliopiga kura theluthi

**Na Elizabeth Zaya**

MGOMBEA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Bahati Ndingo, ametangazwa mshindi katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mbarali, mkoani Mbeya uliofanyika juzi.

Kwa mujibu wa matokeo yaliyotangazwa jana na Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo hilo, Missana Kwangura, theluthi moja ya wapigakura waliojiandikisha ndio waliopiga kura huku wengine hawakujitokeza.

Akitangaza matokeo hayo, Kwangura alisema wapigakura waliokuwa wamejiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura katika uchaguzi wa jimbo hilo ni 185,836, lakini ni 56,662 tu waliopiga kura sawa na asilimia 30.4. Baada ya kuzihesabu, kura halali zilikuwa 56,095 na 567 zikikataliwa.

Kati ya kura halali 56,095 zilizopigwa kwenye vituo 490, Bahati alipata kura 44,334 huku mshindani wake mkubwa kutoka Chama cha ACT-Wazalendo, Modestus Kirufi akipigiwa kura 10,014.

Uchaguzi huo mdogo wa nafasi ya ubunge kwenye Jimbo la Mbarali ulishirikisha vyama 12. Wengine waliokuwa wanagombea ubunge huo ni Halima Magambo (AAFP) aliyepata kura 336, Osward Mndeva (DP) aliyepata kura 130, Zavely Seleleka (UDP) aliyepata kura 158, Exavery Mwataga (CCK) aliyepata kura 118 na Morris Nkongolo (TLP) aliyepata kura 139.

Pia walikuwapo Mary Daudi (UPDP) aliyepata kura 113, Fatuma Ligania (NLD) aliyepata kura 105, Bariki Mwanyalu (Demokrasia Makini) aliyepata kura 207, Hashim Mdemu (ADC) aliyepata kura 173, Mwajuma Mirambo (UMD) aliyepata kura 113 na Husseni Lusewa (ADA- TADEA) aliyepata kura 155.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) pia ilitangaza jana matokeo ya kata sita za Tanzania Bara zilizofanya uchaguzi mdogo wa udiwani juzi huku washindi wote wakitokea CCM.

Katika Kata ya Nala, Halmashauri ya Jiji la Dodoma, alishinda Helman Masila, Kata ya Mfaranyaki ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea, aliyeshinda ni Kayombo Fabian na Ng'wanza Mathias ameshinda katika Kata ya Mwaniko ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

Wengine ni Peter Massawe aliyeshinda katika Kata ya Old Moshi Magharibi, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Simon Massawe aliyeshinda katika Kata ya Marangu Kitowo, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na Twaibu Ngonyani aliyetangazwa mshindi katika Kata ya Mtyangimbole ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

### ACT YALALAMA

Chama cha ACT-Wazalendo kimesema hakikubaliani na matokeo ya ubunge yaliyotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Mbarali, Kwangura.

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, akizungumza baada ya matokeo hayo kutangazwa jana, alidai:

"Uchaguzi ulikuwa na kasoro nyingi sana. Mosi, msimamizi wa uchaguzi alivuruga sana zoezi la kuapisha mawakala. Maeneo ambayo aliahidi kuja kuapisha mchana alifika usiku.

"Hiyo ilisababisha baadhi ya mawakala wetu na wa vyama vingine wasiapishwe. Lakini hata CCM iliapisha mawakala wachache sana kuliko ACT-Wazalendo. Cha kustaajabisha, asubuhi ya siku ya kupiga kura, CCM ilikuwa na mawakala katika vituo vyote.

"Pili, CCM ilitumia vituo ambavyo mawakala wetu walizuiwa kuweka matokeo ya uongo. Ni jambo la kustaajabisha eneo lenye vyumba vitatu, vyumba vyenye mawakala vina mahudhurio hafifu, lakini chumba ambacho hakina mawakala kinapewa mahudhurio ya asilimia 100 au zaidi.

"Maombi yetu ya kutaka vituo vyote vyenye utata masunduku yake yahesabiwe upya yalipingwa na Msimamizi wa Uchaguzi. Tunatafakari kuangalia hatua za kuchukua ikiwamo kuyapinga matokeo haya mahakamani."

Ado alidai kuwa kasoro zinazojitokeza katika uchaguzi wa marudio zinaitia doa serikali, hasa katika kipindi hiki kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Alisema kuwa Chama cha ACT-Wazalendo kitafanya uchambuzi wa kina wa kasoro zilizojitokeza katika uchaguzi wote wa marudio na kuandaa alichokiita ripoti maalum itayowasilishwa kwa wadau, akiwamo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na jumuiya ya kimataifa.

Mgombea Ubunge wa Mbarali (ACT-Wazalendo), Kirufi, pia alidai uchaguzi ulikuwa na kasoro nyingi na ni muhimu mamlaka zinazohusika ikiwamo NEC zifanyie kazi kasoro hizo.

Pia alisema anasikiliza msimamo wa chama kujua hatua inayofuata baada ya matokeo kutangazwa.

# ZEEA yasaidia kujenga uchumi shirikishi Z'bar

**Na Zuwena Shame**

WAKALA wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA) umesema katika utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi, umefanyia kazi changamoto za wajasiriamali ili wakue na kujenga uchumi shirikishi.

Mkurugenzi Mtendaji wa ZEEA, Juma Mohamed, alibainisha hayo juzi alipozungumza na mwandishi wa habari hizi kuhusu jitihada za kuwainua wananchi kiuchumi kwa kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya malengo ya kuondokana na umaskini tangu kuanzishwa kwa wakala huo. Alisema katika utekelezaji wa shughuli zake, ZEEA inawawezesha wajasiriamali, ikiweka mpangilio mzuri kutatua changamoto mbalimbali na kufikia lengo la kuwawezesha kujenga uchumi shirikishi.

Kwa mujibu wa Mohamed, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuingia katika makubaliano na taasisi mbalimbali zinazotoa fursa zinazowahusu wajasiriamali katika kuwapatia mitaji, mafunzo na kuwatafutia masoko ya bidhaa zao kwa lengo la kuwajengea uwezo na kupata masoko rafiki ya bidhaa ndani na nje ya nchi. Alizitaja taasisi hizo kuwa ni pamoja Mamlaka ya Maendeleo ya Bishara Tanania (TanTrade), Maisha Bora Foundation, Shirika la Misaada la Marekani (USAID) na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS).

"Kupitia makubaliano hayo, taasisi mbalimbali zimeanza kutoa mafunzo kwa watendaji wa wakala kwa ajili ya kuzifanyia kazi changamoto zinazojitokeza kwa wajasiriamali," alisema Mohamed.

Aliongeza kuwa ZEEA imepokea mashine 18 za usarifu wa mazao na matunda zilizotolewa na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) kwa ajili ya kuwasaidia kuwapatia mafunzo wajasiriamali kuzalisha bidhaa zenye ubora.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano ZEEA, Hakimu Kimara, alisema kwa sasa wanaendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali katika wilaya zote, ili kukuza mitaji ya kuendesha biashara zao ambapo hadi kufikia sasa jumla ya Sh. 20,232,616,514 zimeshatolewa. Kati yake, kisiwani Unguja zimetolewa Sh. 12,333,420,608 na Pemba Sh. 7,899,195,906.

Kimara alisema kuwa kiasi hicho cha fedha kimetolewa kwa wanufaika 19,373. Kati yao, 7,527 ni wanaume na 11,846 ni wanawake, hivyo kutanua wigo wake wa utoaji wa mikopo kwa kuwa na mikopo inayotokana na asilimia 10 ya makusanyo ya ndani ya serikali za mitaa.

"Jumla ya wajasiriamali 1,615 wameweza kupatiwa mafunzo mbalimbali ya kuendeleza shughuli zao ambapo wajasiriamali 750 wanaofuga nyuki wamepatiwa vifaa kwa ajili ya kuendeleza mazao ya nyuki kwa lengo la kukuza kipato.

"Katika mwaka mmoja tangu kuanzishwa kwake, ZEEA imeweza kutoa mafunzo haya kwenye vituo vyake vyote vyenye lengo la kulea, kuwakuza na kuwasaidia wajasiriamali katika kuzalisha bidhaa zenye ubora na kujipatia masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema.

Kimara aliongeza kuwa ZEEA imefungua tovuti yake wenyewe ambapo taarifa mbalimbali hurushwa kwa ajili ya kuelimisha na kuitangaza kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao.

Alisema kuwa pia wamekamilisha mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa mikopo ambao utarahisisha utoaji mikopo na kuwa na ufanisi katika ufuatiliaji wa marejesho.



Gari aina ya Toyota Ace lenye namba za usajili T 368 DRU, likivutwa baada ya kutumbukia kwenye mtaro katika barabara ya Morogoro, eneo la Friends Corner Manzese, jijini Dar es Salaam jana. Hakuna mtu aliyeumia katika ajali hiyo. **PICHA: MIRAJIMSALA**

## UMEME WA RATIBA

# Vigogo wajifungia siku tatu kusaka suluhu

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inapanua wigo wa vyanzo vya uzalishaji umeme kutoka utegemezi wa maji, mafuta na gesi hadi kwenye jua na upepo ili nchi iwe mzalishaji mkubwa wa umeme Afrika.

Wakati Waziri Mkuu akitangaza hayo, Naibu wake, Dk. Doto Biteko, amesema serikali imeanza kuchukua jitihada za kupunguza makali ya upungufu wa umeme yanayoendelea katika baadhi ya maeneo nchini.

Dk. Biteko ambaye ni Waziri wa Nishati, amesema viongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) jana walikuwa wamejifungia kwa siku ya tatu, wakitafuta suluhisho la tatizo hilo, lengo likiwa kupunguza maumivu kwa wananchi.

Hayo yalibainishwa na viongozi hao jijini Dar es Salaam jana wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Tano la Kimataifa la Nishati lililowashirikisha mawaziri wa nishati kutoka nchi za Malawi, Uganda na Zanzibar, makatibu wakuu, wawekezaji, wadau wa mazingira na kampuni za uzalishaji nishati zaidi ya 100 kutoka Afrika.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema Tanzania ina miradi saba ya kimkakati inayozalisha nishati ya umeme, mingi ikitegemea nishati ya maji kujiendesha, huku michache ikitumia gesi na mafuta.

Alisema mikakati ya serikali ni kuhakikisha wigo unapanuliwa kutoka katika utegemezi wa maji na kutumia jua na upepo ili kuongeza uzalishaji.

"Ukitegemea maji peke yake, mabadiliko ya tabianchi yanapotokea unakuwa unaathirika zaidi hususani inapotoea ukame. Lakini ukipanua wigo ukaenda kwenye uzalishaji wa umeme kwa kutumia upepo na jua, unakua na uhakika katika uzalishaji," alisema Majaliwa.

Kuhusu kongamano hilo, Majaliwa alisema viongozi washiriki watajadili mikakati iliyoko ya nishati, fursa na namna ya kukabiliana na matatizo yaliyoko katika sekta hiyo pamoja na kuwasaidia wajasiriamali katika shughuli za uzalishaji.

Alisema pia watajadili namna ya kuongeza uzalishaji umeme kupitia nishati mbadala na kukabiliana na tatizo la upungufu wa umeme katika nchi zao.

**DK. BITEKO**

Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu, Dk. Biteko, alisema sekta ya nishati inachangia asilimia kubwa katika ukuaji uchumi wa Tanzania.

Alisema kwa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara, zaidi ya wananchi bilioni 0.9 hawana nishati safi ya kupikia. Asilimia 7.8 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia.

Dk. Biteko alisema: "Ripoti iliyotoka hivi karibuni inasema Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi. Hivyo ni lazima tuhakikishe upatikanaji wa umeme wa uhakika unakuwapo."

Alisema Tanzania imejipanga kuhakikisha sekta ya nishati inakuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa na wananchi wanaongeza kipato na ukuaji wa uchumi.

"Tupo hapa leo tunajadili nishati, nishati ambayo Watanzania ukiwauliza watasema ni umeme. Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais (Dk. Philip Mpango) na Waziri Mkuu mmenielekeza kwa muda mrefu tangu nimeteuliwa kwamba tufanye kila tunaloweza tuhakikishe maumivu ya upungufu wa umeme tunayapunguza," alisema.

**VIGOGO TANESCO**

Dk. Biteko alisema serikali inafahamu ukuaji wa uchumi ni mkubwa kwa Watanzania, lakini vyanzo vya umeme ni vilevile, hivyo ni lazima kuongezwa vyanzo vingine vya nishati hiyo ili kuwe na uhakika wa shughuli za uchumi.

"Jana (juzi) tu imetoka ripoti kwamba kati ya nchi zinazokua kiuchumi, Tanzania na sisi tupo. Na ndiyo maana (Waziri Mkuu) katika mkutano huu baadhi ya watu wetu wa nishati tumewaambia wasije, tunataka umeme.

"Mkurugenzi wa TANESCO hatakuwapo na wenzake, wako sehemu kwa muda wa siku tatu, tunafanya ili kupunguza makali ya upungufu wa umeme.

"Hivyo, niwatoe hofu Watanzania kwamba tunafanya kila tunaloweza kuhakikisha upatikanaji umeme unakuwa wa uhakika.

"Na hili ni suala la mpito ndani ya kipindi hiki ambacho Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP) linakamilika, tutakuwa na njia mbadala ya kuondoa mgawo," aliahidi.

**GESI, DHAHABU**

Mmoja wa washiriki wa mkutano huo ambaye ni Mwenyekiti wa Kampuni ya Dodsal, Dk. Rajen Kilachand, alisema wamegundua kuwapo gesi katika eneo la Ruvu mkoani Pwani yenye ujazo wa futi trilioni 3.9.

Alisema pia wamegundua kuwapo dhahabu wakia 100,000 katika eneo la Itingi wilayani Songea na uchimbaji unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwaka huu.

# Anna Henga: Sheria ya Ndoa suala la wakati tu, shida matundu ya vyoo

• Achukizwa na udhalilishaji kupitia utani wa jadi uwanjani, tabia ya ulawiti inavyotapakaa...

**Na Waandishi Wetu**

*TOLEO la jana la gazeti hili lilikuwa na ufafanuzi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, akianika utashi wake unavyompokea Mkuu wa Nchi, Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ni mwanamama mwenzake, hali kadhalika akasimulia anavyomudu nafsi yake katika jamii; ukuu wa taasisi yake, mwanasheria, mchungaji kanisani na mama nyumbani. Je, leo ana nini? Pata ufafanuzi...*



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga. **PICHA: MTANDAO**

**Swali: Kuna kesi zozote kutoka kwa wanamichezo kunyanyaswa kijinsia?**

**Dk. Anna:** Ninadhani ushabiki ndio una changamoto kubwa zaidi kwenye atakayefungwa ndio anakuwa mke. Utasikia nani kamuoa mwenzake? Kwahiyo, yule anayeshindwa ndio anakuwa mwanamke na ndiye aliyeolewa na timu.

Ni vitu vinavyoonekana vizuri, lakini ni udhalilishaji mkubwa sana wa haki za wanawake na wengi huwa hawafikirii kwa mrengo huo.

Kwa upande wangu, mimi ni mfuatiliaji mzuri sana wa soka na ni shabiki wa Klabu ya Simba. Lakini huwa nikifika kwenye haki, huwa siangalii timu.

Vitendo hivi vimekuwa vikifanyika na timu zote mbili pale ambapo wanadhalilisha timu fulani kwa sababu ya ushabiki, ni kitu ambacho hakipendezi.

Hivi karibuni kumekuwa na unyanyasaji wa watu wenye ulemavu wa ngozi na kesi ya binti mwenye jinsia tata. Sitaielezea kwa sababu ni changamoto inayotakiwa kushughulikiwa kitabibu zaidi.

**Swali: Vyombo vya habari ni marafiki katika majukumu yenu. Mnashirikiana nao vipi kufanikisha mnayoyafanyia kazi?**

**Dk. Anna:** Tukio letu la kwanza la kimkakati katika taasisi yetu linahusu elimu kwa vyombo vya habari na bila wao, sisi tusingekuwa hapa tulipo na kazi isingekuwa nyepesi kwa sababu vinawafikia watu kwa haraka zaidi na nina heshimu sana vyombo vya habari.

Ninaamini ukiita watu wachache na kuzungumza nao ni tofauti na utakapoita vyombo vya habari kwa kuwa taarifa ile itawafikia watu wengi zaidi.

**Swali: Umewezaje kuwa chanzo bora cha habari kwa vyombo vya habari?**

**Dk. Anna:** Vyombo vya habari ni sauti na ninaamini katika ninachokiongea. Hiyo ni moja. Pili; ninaviamini sana vyombo vya habari kwa sababu ni sauti ya jamii na kwa upande mwingine kama utani wanasema ni mhimili wa nne wa dola.

Kuna wakati nilisema sitakaa nikatae chombo cha habari kwa sababu kulikuwa na utafiti unaonesha waandishi wa habari wanawake ni wachache, nikasema kama kuna vitu vya kuongea kwanini nisiongee?

Labda niwe ninaumwa au nimeshindwa kuzungumza na hii imenifanya niwe bora kadri ninavyozidi kuzungumza, ninazoea na siogopi kabisa.

**Swali: Mahakama iliamuru serikali ifanye marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, lakini hadi sasa kuna ukimya katika hili. Wanaharakati wa haki za binadamu mmebariki ukimya huu?**

**Dk. Anna:** Tulifanya kampeni nyingi, uelimishaji na kesi tulifungua na mwenzetu Rebecca (Gyumi) ambaye ni mjumbe wa bodi na tulimpa wakili na tumeendelea kusisitiza sheria hii ibadilishwe.

Ahadi ya mwisho ambayo tulipata kutoka kwa Waziri wa Sheria na Katiba (kipindi hicho, Dk. Damas Ndumbaro) ni kwamba utapelekwa muswada bungeni mwezi wa tisa (Septemba) mwaka huu. Kwahiyo, na sisi tunasubiri muswada huo.

Lakini harakati zilianza muda mrefu sana. Sheria ya Ndoa kuruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa si sawa, ni mdogo sana kuwa mke wa mtu na kuchukua majukumu ya ndoa.

Kwa kipindi kile hiyo sheria ilikuwa halali kutokana na hali ilivyokuwa, lakini kwa sasa miaka 14 ni ya mtoto kuwa shuleni na mpaka amalize chuo ni zaidi ya miaka 10 ijayo ndipo anaweza kuchukua majukumu ya ndoa.

Sheria hiyo ni kandamizi na tunaamini mpaka waziri atatuletea muswada wa kuirekebisha

**Swali: Kwa sasa watoto wa kike wamekuwa wanapata haki yao ya kwenda shule za awali na msingi, lakini wanapomaliza darasa la saba hasa kwa vijijini, wazazi wamekuwa wazito kuwaendeleza. Mnalishughulikia vipi hili?**

**Dk. Anna:** Ni swali zuri sana umeuliza. Sisi kama Watanzania tumevuka malengo ya Umoja wa Mataifa ya kuandikisha watoto wa kike, yaani watoto wa kike wanakuwa wengi shuleni.

Lakini changamoto ni kuwa kadri madarasa yanavyoongezeka, idadi yao inazidi kupungua. Sisi sio watu wa elimu, hivyo tumeona tuwaachie watu wanaoshughulikia masuala ya elimu watetee.

Hata hivyo, katika ripoti yetu huwa tunaonesha changamoto ya elimu kama haki ya binadamu na tunaonesha kwanini watoto wa kike wanapungua shuleni. Kwa mfano, katika ripoti yetu ya mwaka 2022, tumeonesha masuala ya matundu ya vyoo na kuonesha kwa jinsi gani tundu la choo linasababisha mtoto kuacha shule.

Unakuta shule ina vyoo vyenye matundu manane; manne kwa wanawake na manne mengine kwa ajili ya wanaume, kitu ambacho hakitakiwi kiuhalisia. Wanawake wanahitaji matundu mengi zaidi kwa sababu ya maumbile yao.

(Uwiano unaotakiwa kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, ni 1:20 yaani tundu moja kwa kila wasichana 20 na 1:25 kwa wavulana).

Wanafunzi wa kike pia wanahitaji sehemu za kujihifadhi wanapokuwa katika hedhi na vifaa ambavyo ninafikiri shuleni hakuna. Kwahiyo, vitu kama hivyo tunatetea kupitia haki za binadamu ili serikali na wizara husika watatue changamoto hizo ili mtoto wa kike asiishie njiani kielimu.

**Swali: Lugha ya matusi na udhalilishaji vimeshamiri katika mitandao ya kijamii. Nini kifanyike kukabili hali hiyo?**

**Dk. Anna:** Mitandao ya kijamii ni mizuri hasa pale unapoitumia vizuri, lakini kuna ambao wanaitumia vibaya hasa kuchafua jinsia ya kike, na huwa ninawashauri wanawake kuwa ukitaka kuwa kiongozi, jiandae kisaikolojia kukabiliana na changamoto yoyote itakayojitokeza kupitia mitandao hiyo.

**Swali: Mara nyingi idadi ya wanawake ni kubwa kwa namba, lakini katika kuzungumzia changamoto zao idadi inakuwa ndogo. Unadhani elimu haiwafikii vya kutosha?**

**Dk. Anna:** Hili suala ni la kihistoria, ni suala la tamaduni zetu ambazo tunajaribu kupambana nazo na utamaduni haubadiliki kirahisi. Mwanamke aliwekwa pembeni.

Hata ninyi waandishi wa habari wanawake sasa hivi mmeanza kuwa wengi. Kipindi cha nyuma walikuwa ni mmoja mmoja, hata taarifa ya habari anapoonekana mwanamke tulikuwa tunashangaa. Walikuwa kama kina Eda Sanga na mwingine alikuwa anatangaza mpira, tulikuwa tunashangaa.

Wanawake waliwekwa pembeni, mtu akizaa mtoto wa kike na wa kiume, wa kiume tu ndiye aliyekuwa anapelekwa shuleni, lakini kwa sasa tunapelekwa shuleni kwa usawa, tena wanawake ni wengi zaidi. Angalau tunaanza kukua vizuri zaidi.

Lakini elimu hiyo inawafikia vipi hao wanawake? Sisi (LHRC) tulifanya utafiti kwanini vituo vyetu vya kisheria wanawake ni asilia 37 tu. Tukagundua hata tunavyowafikia kwa kutumia mitandao ya kijamii, wanawake wangapi wanatumia simu janja?

Tunatumia Kiganjani App ambayo ipo kwenye simu janja, je ni wanawake wangapi taarifa zinawafikia?

Tukaja na mkakati unaitwa Mobile Clinic mfano, tunakwenda mahali kama sokoni tunawaita watu waje watusikilize 'jamani njooni msikilize haki zenu hapa'. Kwahiyo, tunawafikia wanawake wengi zaidi.

Mbinu tunazozitumia kwa sasa watu wa jinsia wanaita ujumuishaji wa jinsia ambapo tunahakikisha kila kundi tunalifikia kwa namna yake. Imekuwa rahisi zaidi kuwapata wanawake kwenye kujitetea.

**Swali: Mmewahi kupokea kesi za ulawiti kwa watoto wa kiume?**

**Dk. Anna:** Kesi za ulawiti hasa kwa watoto wa kiume ni nyingi sana, na miongoni mwa kesi ambazo tunazipokea sisi na tunazoziandika katika ripoti zetu za haki za binadamu, zinazoongoza za ukatili dhidi ya watoto, ukatili dhidi ya wanawake kisha makundi mengine.

Kwa upande wa kundi la watoto, ulawiti hasa watoto wa kiume, kesi zao zinaripotiwa kwa wingi zaidi. Katika ripoti yetu ya haki za binadamu kwa miaka mitatu mfululizo, imeonesha kiwango hicho kwa takwimu kabisa.

***Imeandaliwa na Mwanahamisi Mussa na Emmaloveness Gaston (TUDARCo).***

# Madeleka aungana na familia kumshtaki IGP

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MAOMBI madogo ya jinai namba 28/2023 baina ya James Sije dhidi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) kuhusu kushikiliwa kwa kijana (mleta maombi ) kwa zaidi ya miaka miwili bila kuonekana, yamemwibua Wakili Peter Madeleka Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza kutetea wanafamilia ili kupatiwa haki yao.

Katika shauri hilo, mshtakiwa mkuu ni ofisi ya IGP. Washtakiwa wengine ni ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Mwanza, Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Nyamagana na Mkuu wa Kituo cha Polisi Nyamagana.

Licha ya shauri hilo lililoitwa kwa amri ya mahakama kwa ajili ya kusikilizwa jana chini ya Jaji Lilian Itemba, upande wa Jamhuri uliomba liahirishwe kutokana na wakili wake anayesimamia shauri hilo kuwa nje ya kazi kwa dharura ya kifamilia.

Akiwasilisha ombi la kuahirishwa kwa kesi hiyo, Wakili wa Serikali, George Ngemera, aliyewakilishwa na Wakili Evance Kaisi, alisema upande wa Jamhuri hauko tayari kusikiliza shauri hilo kutokana na wakili anayehusika kuwa na msiba mkoani Kagera.

Ombi hilo lilipingwa vikali na Wakili Madeleka aliyedai kuwa hoja hiyo haina mashiko kisheria kutokana na washtakiwa kuwa ni taasisi za umma ambazo haziwezi kufiwa na kuomba mahakama kulitupilia mbali.

Licha ya pingamizi hilo, Jamhuri iliwasilisha ombi lingine la kupewa siku 14 kwa ajili ya kuwasilisha kiapo kinzani. Ombi hilo pia lilipingwa na upande wa walalamikaji kwa madai kuwa tangu wapokee nyaraka za kesi hiyo ni zaidi ya mwezi, hivyo walitakiwa kutumia muda huo kukamilisha matakwa yote ya kisheria.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, Jaji Itemba alikubaliana na hoja za upande wa Jamhuri na kutoa siku tatu kuwasilisha kiapo kinzani.

Jaji Itamba aliahilisha kesi hiyo hadi Septemba 25, mwaka huu kwa ajili ya shauri hili kusomwa na kusikilizwa.

Akizungumza nje ya mahakama, Wakili Madeleka alieleza msingi wa maombi hayo ni kwamba Agosti 17, 2021 mleta maombi, James Sije, alikamatwa na askari polisi watatu wakiongozwa na Sajenti Msobi Mageni na tangu kukamatwa kwake, hajawahi kuonekana popote.

Pia alidai kuwa jambo hilo lilileta simanzi kwa familia kwa kuwa muda wote huo, hawajui hatima ya kijana wao na kwamba familia hiyo kupitia baba mzazi wa kijana, Willium Sije, ilifuatilia katika taasisi mbalimbali bila mafanikio.

Baada ya kukosa msaada kutoka taasisi hizo, alidai kuwa familia iliona vyema kutafuta haki ya kijana huyo katika mahakama chini ya kifungu cha sheria 360 (I) 'a' na 'b' cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai lengo ili kuiomba mahakama kutoa amri kwa wanaomshikilia kinyume cha sheria na kumfikisha katika vyombo vya sheria kama atakuwa na mashtaka ili sheria ichukue mkondo wake.

Pia alidai kuwa kwa mujibu wa shauri hilo, kama hatakuwa na tuhuma zozote zinazomkabili, aachiwe uhuru kwa kile alichodai kuwa kwa mujibu wa Ibara ya 15 (i) na (ii) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila mtu anastahili kuishi huru.



Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Noel Mbonde (kulia), akibadilishana nyaraka na mwanzilishi wa asasi inayotoa misaada ya elimu ya GFP, Michael Vallez, baada ya kutiliana saini mkataba, Dar es Salaam jana, ambapo walimu wa vyuo vya VETA watapelekwa kusomea uchomeleaji vyuma Marekani na Afrika Kusini. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Watoa angalizo mkataba mpya Bandari bei bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Wachukuzi Bandarini Zanzibar, umehadharisha kuwapo hatari ya mfumuko wa bei za vyakula, viungo na matunda iwapo tozo mpya ya ushuru iliyowekwa na wawekezaji wanaoendesha Bandari ya Malindi, hautaangaliwa upya.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imeipatia Kampuni ya African Global Logistics (AGL) ya Ufaransa kwa ajili ya kuendesha Bandari ya Malindi kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Wakizungunza jana na waandishi wa habari, viongozi wa umoja huo walisema hali hiyo inaweza kujitokeza kutokana na mgomo wa wachukuzi wa mizigo, ulioanza kujitokeza tangu kuanza kutumika tozo mpya za ushuru zilizotangazwa na mwekezaji huyo.

Kaimu Mwenyekiti wa Umoja huo, Masoud Haji Juma, alisema tozo hizo zimetangazwa ghafla bila wadau kushirikishwa. Alisema viwango hivyo ni vikubwa na kama vitatumika, vitaathiri biashara za vyakula zinazoingizwa kutoka nje ya Zanzibar.

"Mtoto anapozaliwa familia hukaa pamoja na kupendekeza jina lakini mwekezaji huyu amekuja kuendesha shughuli za bandari bila sisi wadau kushirikishwa zaidi ya kuarifiwa kuwa AGL itaanza kazi Septemba 18, mwaka huu," alisema.

Masoud alisema mfumuko wa bei utaathiri wananchi wote kwa kuwa bidhaa za nafaka, matunda na viungo ni mahitaji ya lazima ya kila siku kwa wananchi wa Zanzibar.

"Wakati Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi anafanya kampeni, alikuja na kukutana na wadau wa bandari na kuahidi mambo yatakuwa mazuri katika kuendeleza biashara zao lakini sasa tunashuhudia tozo zikiongezeka kwa asilimia 100 mpaka mizigo tunashindwa kuitoa na kubaki katika majahazi. Hii kuna hatari ya mizigo kuoza," alisema.

Pia alisema kutetereka kwa biashara kutaathiri hata ukusanyaji wa mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania Tanzania (TRA), hivyo kuwataka viongozi kukaa ili kupata mwafaka.

Alisema kabla ya AGL kukabidhiwa uendeshaji wa bandari, magari ya mizigo yalikuwa yakipata kibali cha mwaka lakini utaratibu huo umefutwa na magari yote kutakiwa kila yanapoingia na kutoka.

"Bandari ya Malindi ndiyo bandari, zingine bandari nne zilizobakia ni vituo vya bandari zikiwamo Mkokotoni, Mkoani, Wete na Weshia na hii Malindi ndiyo nguzo ya uchumi wa Zanzibar," alisema.

Naye Kiongozi Mwandamizi wa Jumuiya ya Wachukuzi, Omar Makame Mtumweni, alisema kikao cha pamoja cha wanachama kimeamua kupitisha azimio la kukutana na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) baada ya wachukuzi kugomea tozo mpya zilizotangazwa na mwekezaji.

"Jambo hili ni zito linahusu uhai wa biashara. Tumeamua kukutana na Mkurugenzi wa Shirika la Bandari kwa sababu wenzetu wameanza kazi kimyakimya bila kutushirikisha wakati sisi ndio wadau wakuu wa shughuli za bandari," alisema.

Alisema tozo za utoaji mizigo bandarini zimeongezeka kwa zaidi ya asilimia 100. Alitoa mfano wa sasa kwamba tani sita zinalipiwa Sh. 210,000 wakati awali ilikuwa Sh. 77,000 wakati tani nne sasa zinatakiwa kulipiwa Sh. 156,000 badala ya Sh. 52,000.

Mjumbe wa Jumuiya ya Amana Zanzibar, Subira Ambari Ali, alisema waathirika wakubwa wa mgomo huo ni wanawake wanaojishughulisha na uwakala wa usafirishaji mizigo baada ya mgomo huo kudumu kwa siku ya nne hadi jana.

Alisema kazi hizo ndizo zinazowafanya kuendesha familia zao lakini tangu juzi wanakwenda na kurudi wakiwa mikono mitupu baada ya wachukuzi kugomea tozo mpya.

"Tunaomba serikali iangalie upya viwango vya tozo kunusuru wafanyabiashara wadogo wanaoingiza bidhaa za vyakula kama maharage, mchele, viazi mbatata, viungo na matunda, ikiwezekana kurejesha viwango vya zamani," alisema Subira.

Ofisa uhusiano wa ZPC, Hassan Amour, alisema viwango hivyo vya tozo si vipya bali vilikuwa havitumiki ili kuwapa unafuu wafanyabiashara na wananchi.

"Tozo hizi si mpya zipo hata kabla ya kuja mwekezaji lakini zilikuwa hazitumiki. Walipokuja wawekezaji hawa walitaka wapewe nyaraka zote za uendeshaji wa bandari vikiwamo viwango vya tozo kabla ya kuanza kuzitumia," alisema.

Uendeshaji wa Bandari ya Malindi umekabidhiwa kwa AGL kwa muda wa miaka mitano kuanzisa Septemba 18, mwaka huu.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Ratiba ya upatikanaji umeme izingatie muda maeneo husika*

**KUTOKANA** na ukosefu wa mvua katika maeneo mengi nchini, kumesababisha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuweka ratiba ya upatikanaji wa nishati hiyo baada ya upungufu wa uzalishaji katika vyanzo vyake.

Inapotokea mvua kuchelewa kunyesha au kukosekana katika baadhi ya mikoa, huathiri uzalishaji wa umeme katika vyanzo kutokana na mabwawa ya kuhifadhia maji kupungua kina cha uzalishaji.

Hali hiyo husababisha Tanesco kushindwa kutoa huduma hiyo ipasavyo na baadhi ya maeneo kukosa nishati hiyo.

Tunajua wafanyabiashara wengi wanategemea umeme ili biashara zao ziende vizuri na pia wazalishaji viwandani ni tegemeo lao kubwa nishati hiyo.

Tanesco imetoa ratiba rasmi ya upatikanaji wa nishati hiyo katika maeneo yaliyotajwa ukiwamo Mkoa wa Dar es Salaam ambo ni mji mashuhuri wa biashara na unaotegemewa kwa uchumi.

Wawekezaji wengi wamewekeza katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu ndio mji wa kibiashara ambao huingiza watu wa mataifa mbalimbali kufuata bidhaa.

Ratiba iliyotolewa na Shirika inaonesha baadhi ya maeneo umeme utakatwa kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 12 jioni na sehemu nyingine ni kuanzia saa 12 jioni hadi saa sita usiku.

Muda huo ni mwingi kwa watu wanaotegemea umeme kufanya uzalishaji, lakini kutokana na hali halisi ya upatikanaji wa mvua inabidi wakubaliane na ratiba hiyo.

Ombi kubwa kutoka kwa wananchi ni uzingatiaji wa ratiba hiyo, kama imepangwa kutokuwapo saa mbili asubuhi hadi saa 12 jioni, iwe hivyo.

Isije ikawa unakatwa saa 12 asubuhi mpaka saa tatu usiku umeme haujarudishwa na kuleta kero kwa wananchi.

Baadhi wa watu hununua vyakula na kuvihifadhi kwenye majokofu ili kwenda na bajeti anayojipangia mtu.

Ratiba isipofuatwa inaweza kumwathiri kwa kufanya vyakula alivyovihifadhi kuharibika na kuleta hasara kwake.

Vile vile, ratiba ya usiku ingerekebishwa ili maeneo yasikae kwenye giza kwa muda mrefu. Kipindi hicho ndicho watu wasiokuwa na nia njema, hukitumia kuvamia nyumba na kufanya wizi. Baadhi ya maeneo ambayo yamepangwa kwenye ratiba hiyo ni Kinondoni Kusini, Kaskazini na Temeke ambapo inaonesha imeanza kuanzia Jumapili na itakwenda hadi Jumamosi ya wiki hii.

Taarifa iliyotolewa na Tanesco inaonyesha endapo eneo moja litakosa huduma ya umeme kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 12 jioni, siku inayofuata litakosa huduma hiyo kuanzia saa 12 jioni hadi saa sita usiku. Pia ratiba hiyo imehusisha Mkoa wa Iringa.

Ufafanuzi wa Tanesco ulitolewa mwishoni mwa wiki hali hiyo ya ukatikaji umeme siyo mgawo, bali inatokana na upungufu wa huduma hiyo katika vyanzo vya uzalishaji.

Ni kweli hali ya upungufu wa umeme inarudisha nyuma shughuli za uzalishaji kwa sababu wengi hutegemea kwa ajili ya kujiingizia vipato.


Wazalishaji wengine hulazimika kutumia majenereta ili kuendelea na kazi zao hali inayowasababisha kuingia gharama kubwa ya uzalishaji na matokeo yake huamua kuongeza bei kwenye bidhaa zao ili kufidia gharama.

Tunategemea kuwa tatizo hili litakuwa la muda mfupi, kutokana na utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), kutabiri mvua kubwa kunyesha nchini.


Ingawa imetabiriwa inaweza kuleta madhara, lakini ikitumika kuhifadhi maji itasaidia kuondokana na tatizo hilo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tamary George

# *Umma tuwe makini na matumizi ya akili zetu, maisha ya kila siku*

**YALIYOMO** katika dunia tunayoishi sasa, mengi ni zao la mawazo yetu na dhamira ambazo huzaa matendo. Kama tunayoyaona ni mazuri au mabaya, ni zao la matendo yetu.

Hivyo, tuwe makini na matumizi ya akili zetu, tuzitumie vizuri kuleta manufaa kwa jamii, sio maangamizi kuleta amani na sio mifarakano. Yote ni kuwezesha kuleta umoja na si utengano.

Mtu ambaye hawezi kuongoza mawazo yake, ni vyema ajitafakari zaidi. Akili zetu ndio kiongozi wetu hutuongoza kwenye mabaya au mema.

Kitu kinachosababisha kuwa na matumizi mabaya ya akili yanatokana na matatizo ya kisaikolojia kama vile hofu, wasiwasi na magonjwa mengine ya akili ambayo yanatokana na kuathirika na kitu ambacho hakikutegemea kutokea, mfano mzuri ni taarifa za mshangao kama vifo, ajali, ukatili wa kijinsia kwa wanawake.

Pia matumizi ya dawa za kulevya na pombe zinakuwa na mwongozo mkubwa wa kumfanya mtu apoteze usahihi wa akili yake, akaangukia kufanya yasiyotarajiwa.

Mara nyingi watumiaji dawa za kulevya na pombe, wanasababisha kuathiri uhusiano wa mtu mmoja na mwingine, hatua ya kuingiza katika matatizo ya kisheria.

Matumizi mabaya ya akili yanakaribisha magonjwa ya akili kama vile ambazo zinachangia msongo wa mawazo kwa mama mjamzito, kuumia mgongo, ukatili wa kingono, vyote vikiibua vyanzo vya mtu kuchanganyikiwa; kimwili, kimazingira na kijamii, hatimaye ugonjwa wa akili mtu anajidhuru.

Pia kunapokuwapo mazingira mabaya kama vile ukosefu wa usalama, umaskini na kukosekana fursa za kiuchumi, kama matatizo ya fedha kwa mtu, msongo wa mawazo, vyote husababisha ukiukwaji wa matumizi mazuri ya akili ya mtu.

Kuna njia ambazo kama binadamu tunapaswa kuwa makini na matumizi ya akili zetu, kwa sababu kwanza tunapaswa kujua akili zetu zina nafasi ya kuathiri uhusiano wetu na watu wengine, hasa ikiwa tunafichua siri zao bila ya idhini yao.

Akili hizo zinasababisha hisia na hatua za kuona aibu na zinaweza kuathiri afya zetu za akili, hata athari za kisheria, ikiwa tunafichua habari ambazo zinaweza kutufanya tuwe hatua ya uhalifu.

Tunapaswa kuzingatia matumizi ya akili, nani tunamwambia siri zetu na kuhakikisha tuna uhakika, kwamba hatufichi habari yoyote, kinyume chake inaweza kutufanya tuwe na hatia ya uhalifu.

Pia kwa kuzingatia athari za afya ya akili ambazo zinaweza kusababishwa na hisia za aibu, ikiwa inachangia katika athari za kisheria.

Madaktari wana mchango mkubwa katika kuwaomba watu wawe makini na matumizi ya akili, wakiwajibika kuwatibu na kuwapa elimu mbalimbali ya akili. Mfano wa wajawazito mara nyingi wakienda kliniki, wanashauriwa wasiwe wanachosha akili kufikiria mengi magumu.

Vilevile, watumiaji wa dawa za kulevya na watumiaji pombe wakienda kwa madaktari, huwa wanashauriwa wasiwe wanajipa mawazo sana kufikia hatua ya kutumia hivyo vilevi.

Serikali pia ina mchango mkubwa katika kuwajibika kutoa elimu kwa wananchi wake, kuhusu masuala yanayohusu afya ya usalama na ustawi wa jamii, mfano nchini serikali inajihusisha na masuala ya afya na hospitali, ambazo kwa heshima yake Rais Mama Samia Suluhu Hassan, wananchi wanamshukuru amewawezesha kuwasaidia kupitia halmashauri za mikoa mbalimali zinajenga baadhi ya vituo vya afya.

Elimu hiyo inayotolewa, inalenga kuwaelimisha wananchi kuhusu wagonjwa mbalimbali na jinsi ya kujikinga nayo na kutunza afya zao.

Hivyo ni muhimu kuzingatia kanuni za usalama, wakati wa matumizi yake mfano muhimu ni kufuata maelekezo yaliyopo kwenye lebo ya bidhaa husika na kutumia bidhaa hiyo kulingana na maelekezo hayo.

HABARI KITAIFA

## Matinyi: Kukosekana urasimishaji ardhi tatizo

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Wilaya ya Temeke, Mobhare Matinyi, amesema suala la miliki ya ardhi katika nchi linatokana na kukosekana mfumo na utaratibu mzuri wa kurasimisha umiliki.

Matinyi aliyasema hayo jana wilayani Temeke wakati wa uzinduzi wa kliniki ya ardhi kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP), unaolenga kutoa hati papo hapo kwa wananchi.

Mradi huo unaotekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Watu na Makazi, umefadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), Sh. bilioni 345.

Akizungumza katika uzinduzi wa utoaji wa hatimiliki kidigitali kwa wananchi wa Mtaa wa Mbagala Kuu Mashariki, Matinyi alisema kadhia ya umiliki husababisha mvutano wakati watu wakifuatilia mirathi.

"Hivi tunaongea hapa humu humu ndani ya Wilaya ya Temeke kuna migogoro ya miradi na kisa kikubwa aliyekuwa anamiliki wakati akiwa hai hakurasimisha umiliki huo ama hakujua afanye nini au hakujali au pengine kulikuwa na udhaifu fulani katika mfumo. Tuna usumbufu mwingi wa aina hiyo," alisema.

Pia mtu anapotaka kujenga, kupata vibali ni tatizo na anayetaka huduma ya mkopo kwa taasisi za kifedha, huzikosa kwa kuwa kuna tatizo kwenye kurasimisha umiliki wake.

Alisema wizara imeamua kuja na mradi huo ambao ili ufanikiwe kama miradi mingine, kuna haja ya kuwa na wataalamu, mipango mikakati na fedha.

"Tutoe pongezi za dhati kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake, aliwafikia wadau muhimu wa maendeleo Benki ya Dunia (WB) na kuwezesha kupatikana Sh. bilioni 345 nchini. Huduma zote zinatolewa kidigitali," alisema.

Alisema eneo mojawapo muhimu lenye uhusiano wa moja kwa moja na masuala ya kurasimisha ardhi ni kuirasimisha sekta ya biashara ambayo Wilaya ya Temeke ina kilometa za mraba 240 na ina idadi kubwa ya wananchi milioni 1.4.

Alihamasisha wananchi kujitokeza katika mchakato huo wa kurasimisha ardhi ili kupata hatimiliki ambazo zitawasaidia kuendesha maisha yao na kukua kiuchumi.

Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam, Rehema Mwinuka, alimshukuru Rais Samia kwa kutafuta fedha hizo ili kutekeleza mradi huo ambao unaachana na majalada na kuwafikia wananchi kidijitali popote walipo.

Mwinuka aliwaomba wananchi wenye migogoro midogo midogo waliyoipeleka mahakamani, wayatoe huko ili waweze kuishughulikia kwa kuwa mradi huo una hatua mbalimbali ikiwamo kutoa elimu, hati na kubadilisha taarifa.

# CRDB yatunukiwa tuzo huduma za Kiislamu Afrika Mashariki



Mwenyekiti wa Global Islamic Finance Awards (GIFA), Prof. Humayon Dar (kushoto), akikabidhi tuzo ya huduma bora zinazofuata misingi ya dini ya kiislamu 'the Best Upcoming Islamic Banking Window 2023' kwa Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na wa Kati Benki ya CRDB, Bonaventure Paul (kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Benki za Kiislamu Benki ya CRDB, Rashid Rashid, iliyotolewa katika hafla ya 13 ya Global Islamic Finance Awards jijini Dakar, Senegal hivi karibuni. **PICHA: CRDB**

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache baada ya kuzindua kadi za Akaunti ya Al Barakah, Benki ya CRDB imekuwa benki ya kwanza katika ukanda wa Afrika ya Mashariki kutunukiwa tuzo ya ubora katika huduma za benki zinazofuata misingi ya sheria mwaka 2023 katika hafla ya 13 ya Tuzo za Global Islamic Finance Awards (GIFA) zilizofanyika jijini Dakar, Senegal.

Benki ya CRDB imepata tuzo hiyo ikiwa ni miaka miwili tangu izindue dirisha la huduma za kibenki zinazofuata masharti ya Kiislamu "CRDB Al Barakah".

Akikabidhi tuzo hiyo, Mwenyekiti wa GIFA, Prof. Humayon Dar, alisema CRDB inafungua milango kwa taasisi za fedha Afrika Mashariki kuhudumia Waislamu ambao wangefurahi kuhudumiwa kwa misingi ya imani yao.

"Benki ya CRDB ni taasisi ya kwanza ya fedha kushinda tuzo zetu. Tunaamini mtakuwa na mabalozi wazuri wa kulinda dirisha hili muhimu katika huduma za kibenki katika kuhudumia Waislamu katika ukanda huo.

"Tunaamini tutaendelea kushirikiana kufungua fursa zaidi za mitaji na uwekezaji kwa wananchi mnaowahudumia," alisema Prof. Dar.

Benki ya CRDB ilizindua huduma za Al Barakah mwishoni mwa mwaka 2021 na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akawa mteja wa kwanza kufungua akaunti na wiki hivi karibuni benki ilimpa heshima ya kuwa mteja wa kwanza kukabidhiwa kadi ya akaunti hiyo, hivyo kufungua milango kwa zaidi ya wateja 70,000 ilionao mpaka sasa.

Mpaka sasa, tayari benki imekopesha zaidi ya Sh. bilioni 90 kupitia dirisha hilo huku ikipokea amana zenye thamani ya Sh. bilioni 85 nchini kote.

Akipokea tuzo hiyo, Paul alisema inawatia moyo kuona kwamba ubunifu wanaoufanya unatambulika kimataifa, hivyo akaahidi wataendeleza ili kukidhi mahitaji na matarajio ya wateja na wawekezaji wanaowapa huduma nchini na nje ya nchi ambako Benki ya CRDB inatoa huduma zake.

"Sisi ndio benki ya kwanza kutoa Islamic banking (huduma za kibenki kwa misingi ya Kiislamu) kupitia mtandao mpana zaidi. Huduma zetu zinapatikana katika matawi yetu yote 260. Washindani wetu wanahudumia katika maeneo machache, lakini sisi tunafika kwenye mikoa yote," alitamba Paul.

Ukiacha Zanzibar na mikoa yenye idadi kubwa ya Waislamu ikiwamo Tanga, Kigoma, Mtwara, Lindi na Tabora pekee, ambako Benki ya CRDB imejielekeza, Paul alisema huduma za Al Barakah zinapatikana hata kwa mikoa yenye idadi ndogo ya waumini wa dini hiyo.

Tuzo hizo za 13 za GIFA zilizoanzishwa mwaka 2011, zilitolewa mbele ya Rais wa Senegal, Macky Sall na kuhudhuriwa na mamia ya washiriki wakiwamo watafiti, wakurugenzi wa kampuni na mashirika ya kimataifa kutoka kila pembe ya dunia kutambua mchango wa washindi wake ambao katika kipindi chote, wanafika zaidi ya 700.


WANATAFUTWA NA POLISI TUHUMA ZA WIZI
ARS/ RB: 8837/2023



JINA : MOSES ALFRED MABULA
KABILA : MSUKUMA WA MWANZA. MAKAZI : DARAJA MBILI ARUSHA UMRI MIAKA :46




JINA : LAZARO RICHARD PYUZA
KABILA : MNYIRAMBA
MZALIWA WA MKOA WA SINGIDA MKAZI WA DARAJA MBILI ARUSHA UMRI MIAKA 37

117600601

Watuhumiwa wa uwizi katika kampuni ya **Predators Safari Club Ltd** iliyopo Arusha maeneo ya Sakina.

***Yeyote atakayefanikisha kutoa taarifa za kukamatwa kwa watuhumiwa hawa zawadi itatolewa ya Tsh:2,000,000/=( milion mbili)***

**Kwa mawasiliano piga simu namba 0767 445344 / 0716 082447 ama toa taarifa kituo cha Polisi.**


## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**






# Ndalichako aagiza taasisi kuwa na wataalamu lugha ya alama

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amezitaka taasisi za umma kutekeleza mwongozo wa kuwa na wataalamu wa lugha ya alama ili watu wenye ulemavu wa kutosikia (viziwi) wapate huduma stahiki.

Prof. Ndalichako aliagiza hayo jana jijini hapa alipotoa maelezo kuhusu maadhimisho ya Wiki ya Viziwi Duniani itakayofanyika kuanzia Septemba 25 hadi 30 mwaka huu mkoani Mbeya ikiwa na kaulimbiu ya 'Dunia ambayo popote walipo viziwi wanaweza kutumia lugha ya alama'.

Alibainisha kuwa serikali imechukua hatua mbalimbali kwa ajili ya mustakabili wa viziwi nchini ikiwamo kuzindua mwongozo wa utekelezaji, ujumuishwaji na umairishaji huduma kwa watu wenye ulemavu Tanzania ambao umeainisha viwango vya ujumuishwaji kwa watu wenye ulemavu.

"Mwongozo huu umejumuisha suala la taasisi za umma kuhakikisha wanakuwa na watumishi wenye ujuzi wa kutumia lugha ya alama ili pale inapohitajika kutoa huduma kwa wateja wenye uziwi, basi pasiwe na kikwazo katika kuwasiliana," alisema.




Waziri huyo alisema ili mwongozo huo utekelezwe, ni lazima taasisi za umma zisizo na watu wa kutafsiri lugha za alama zihakikishe zinakuwa nao ili kuimarisha lugha ya mawasiliano.

Alibainisha kuwa pamoja na jitihada mbalimbali, serikali imedhamiria kila taasisi inayotoa huduma kwa jamii inakuwa na mkalimani wa lugha ya alama na kuwajengea uwezo watumishi wake kuwa na uelewa kuhusu lugha hiyo.

"Kuadhimishwa kwa Wiki hii ya Viziwi Duniani ni mwendelezo wa dhamira ya serikali kutoa fursa za viziwi kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo kwa kushirikiana na jamii inayowazunguka bila kuwapo vikwazo vyovyote vya mawasiliano," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi kuwathamini na kufanya kazi na watu wenye ulemavu kwa sababu wamethibitisha kuwa ulemavu si kikwazo kwao kushiriki katika miradi ya maendeleo.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Taifa (CHAVITA), Adam Shabani, aliishukuru serikali kwa kutoa fursa mbalimbali kwa watu wenye ulemavu huku akishauri kuwapo watafsiri wa lugha za alama katika sehemu za kutolea huduma za kijamii.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (wa tatu kushoto), akitoa cheti kwa Aashim Wadhwa wa LG Electronics baada ya kuibuka banda bora katika maonyesho yaliyoandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (ERB), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Milioni 150/- zatolewa kuwezesha maonesho ya madini na teknolojia

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KATIKA kuendelea kudumisha dhamira ya ubunifu wa kiteknolojia, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imetoa Sh. milioni 150 kudhamini Maonyesho ya Sita ya Teknolojia ya Madini yanayofanyika Geita.

Maonyesho hayo ambayo hufanyika kila mwaka, mwaka huu yanatarajiwa kufanyika kuanzia Septemba 23-30 mwaka huu.

Maonyesho hayo yanafanyika kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) katika viwanja vya Bombambili vilivyoko eneo la Mamlaka ya Maeneo ya Usindikaji Nje (EPZA) mkoani humo.

Akizungumzia ushiriki wa GGML katika maonesho hayo mjini Geita jana, Meneja Mwandamizi wa kampuni hiyo anayesimamia uhusiano wa jamii, Gilbert Mworia, alisema maonesho hayo yamekuwa na mvuto wa kipekee tangu yalipoasisiwa kutokana na ufadhili wa GGML kupitia Mfuko wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR).

Alisema mfuko huo umewezesha ujenzi wa eneo hilo la EPZA pamoja na eneo la uwanja huo wa maonesho.

"Mbali na maonesho, tuliwekeza Sh. milioni 800 katika ujenzi wa jengo la utawala la EPZA. Tunafurahi kuona mpango wetu wa EPZA mkoani Geita unastawi na kutimiza malengo ya jamii ya wana Geita kikamilifu.

"Msaada wetu unavuka usaidizi wa kifedha ambao tumeendelea kuutoa kila mwaka, kwa sababu tulitoa msaada wa maandalizi ya maonesho hayo kama vile mahema, jenereta la dharura na mafuta yanakayotumika kwa wakati wote wa maonesho," alisema Mworia.

Alisema katika kipindi cha miaka sita ya ushirikiano huo na wadau wa maonesho hayo, GGML imeendelea kuelimisha jamii kuhusu teknolojia inayotumika katika vifaa vya uchimbaji madini, hali inayoendelea kukuza uhusiano imara kati yake, kampuni za ndani na wachimbaji madini.

Alisema ili kutimiza malengo ya muda mrefu ya ukuaji wa uchumi endelevu, GGML inaunga mkono Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Mpango huo unalenga kuiwezesha sekta ya uchimbaji madini kukua na kufikia kiwango cha asilimia 10 kwenye Pato la Taifa.

Ufunguzi rasmi wa Maonesho ya Sita ya Madini na Teknolojia mkoani Geita utafanywa na Dk. Dotto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati keshokutwa.

Tarehe 30 Septemba mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kufunga maonesho hayo yenye kaulimbiu 'Matumizi ya teknolojia sahihi katika kuinua wachimbaji wadogo kiuchumi na kuhifadhi mazingira'.

## Wataalamu watunga kanuni za sheria za miji kidijitali

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKUTANO wa wataalamu wa sekta ya mawasiliano duniani unaoratibiwa na Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) kwa ushirikiana Tanzania ujulikanao kama ITU -T SG20 unaendelea jijini hapa.

Mbali na mambo mengine, katika mkutano huo, wanajadili viwango vya kiteknolojia katika teknolojia za kisasa mtandao wa mambo (Internet of Thinks), miji na jamii maridadi (Smart Cities & Communities-SC&C).

Miji maridadi ni watu wanaohusiana na mtandao wa kuvaa miwani ambayo itakuletea ulimwengu wa mtandaoni na kuona ulimwengu halisi.

Pia miji yenye foleni za magari zitatumia kamera na kujua mambo mbalimbali.

Kutokana na mabadiliko hayo kutakuwa na mtandao wa mambo ambao utahusisha vitu, vifaa na huduma ambao utarahisisha utendaji kazi na kuwa na umiliki wa maeneo.

Wataalamu hao wamekutana ili kuweka viwango vitakavyokuwa ndani ya kanuni zitakazosimamia namna teknolojia zitakavyotumika.

ITU -T SG20 ni kikundi-kazi cha Shirika la Kimataifa la Mawasiliano kilichojikita katika sekta ya mawasiliano-pepe (ITU-T).

Dhima ya kikundi kazi hicho ni kusimamia, kuandaa viwango na mapendekezo ya ubora wa mawasiliano pepe yanayotumika duniani.

Aidha, ITU -T SG20 kina jukumu la kutambua na kuorodhesha mahitaji ya viwango vya Mtandao wa Mambo yaani Internet of Things (IoT), kuendeleza na kuidhinisha viwango vya IoT na miji na jamii maridadi na kushirikiana na vikundi vingine vya ITU na mashirika mengine ya viwango ili kuhakikisha viwango vya IoT na SC&C vinakidhi ubora unaokubalika kimataifa.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema juzi kuwa kufanyika kwa mkutano huo nchini ni suala muhimu kwa kuwa limewezesha wataalamu wengi zaidi kuhudhuria na kuleta manufaa kwa nchi.

"Hii ni heshima kwa nchi yetu kupata fursa ya kuandaa mikutano hii ya kitaalamu kwa kuwa kawaida hufanyika Uswisi, wataalamu wetu wengi zaidi wameweza kuhudhuria, suala ambalo ni afya kwa sekta ya mawasiliano nchini kwetu," alibainisha.

Mkurugenzi wa Idara ya Masuala ya Kisekta wa TCRA, Mwesigwa Felician alisema ITU -T SG20 inaangazia maeneo ya IoT, miji na jamii maridadi ili kuhakikisha dunia inaweka matumizi ya teknolojia za kidijitali zenye viwango vinavyotakiwa kwa kuzingatia ukuaji wa kasi wa teknolojia ambao dunia inaushuhudia.



## Uchakavu miundombinu shule za Moshi washtua

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI imeagiza wakurugenzi wa Manispaa ya Moshi na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miradi yakiwamo majengo ya shule za sekondari na msingi yaliyochakaa.

Wilaya hiyo ina shule za sekondari 103 ambazo zinatishiwa na uchakavu kwa asilimia 30 huku shule za msingi zikiwa 229. Kati yake, 90 zinakabiliwa na uchakavu licha ya serikali na wadau kuendelea na ukarabati.

Jana katika uzinduzi wa maabara ya kompyuta ya Shule ya Sekondari Maringeni, Mkuu wa Wilaya hiyo, Kisare Makori, alisema shule nyingi zilizoko katika halmashauri hiyo zimejengwa katika miaka 1940, hali inayochangia kuwa na miundombinu chakavu kwa sasa.

Mkurugenzi wa Tanzania Enlightenment Development Innavation (TEDI), Gloria Anderson, aliomba serikali kuweka nguvu katika miradi mbalimbali ya maendeleo hasa ya elimu ili kukuza elimu katika utandawazi.

"Tumetoa kompyuta mpakato 12 kwa wanafunzi wa shule ya sekondari ili kuboresha elimu yao kwa kuwa wanasoma masomo ya ICT, hii itasaidia kuboresha ufaulu na kusaidia vijana kuingia katika umahiri wa masomo ya kompyuta nchini.

"Tunaomba vifaa hivi vitumike vizazi na vizazi, hatutegemei kuona vinaharibikiwa, walimu na wanafunzi hakikisheni mnatunza vifaa hivyo," alisema.

Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Moshi, Benedect Sandy, alisema tayari katika halmashauri hiyo kumetengwa zaidi ya Sh. milioni 15 kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo na wana ahadi ya fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya maabara ambazo zipo katika hatua za kupaua.

"Halmashauri ya Moshi tuna shule 101 na tunajenga mbili mpya, lakini shule zetu za sekondari zimeanza miaka mingi kuanzia mwaka 1940 na nyingine ni shule zilizojengwa na jamii.

"Hivyo, yako majengo mengine yamechakaa, ingawa serikali inaendelea na ukarabati kulingana na upatikanaji fedha hasa kwa zile kongwe," alisema Sandy.

# Kila watoto wagonjwa 10, wawili wanahara Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Idara ya Watoto Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Salha Rashid, amesema kati ya watoto wagonjwa 10 wanaowapokea, wawili hadi watatu wanakutwa na ugonjwa wa kuhara sawa na watoto 21 kwa wiki na 84 kwa mwezi.

Dk. Rashid alibainisha hayo jana katika mazungumzo mahususi na Nipashe kuhusu ugonjwa wa kuhara kuwakumba watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Alisema hospitali hiyo ilipokea watoto wengi wenye ugonjwa huo miezi miwili iliyopita (Julai na Agosti).

Alisema chanzo cha ugonjwa huo kwa watoto wadogo ni kunywa maji au kula chakula ambacho hakijaandaliwa katika mazingira salama, hivyo kuwa na bakteria, pia watoto wenye utapiamlo na wanaosumbuliwa na kifua kikuu (TB) kutokana na kinga zao kuwa chini.

**Nyonyo zinakuwa hazijaoshwa vizuri kama zinakuwa hazijawekwa kwenye maji ya moto na namna ya kutunza ni tatizo kwa wazazi wengi.**

Dk. Rashid alisema mtoto anatakiwa awe amepata chanjo ya Rota ambayo itamsaidia kutopata maradhi hayo ya kuhara.

Alisema ugonjwa huo wanautibu kwa kuangalia historia ya mtoto kama aliharisha zaidi ya mara tatu kwa siku.

Alisema mtoto akihara kuna hatari kupoteza maji mengi mwilini na ili kumsaidia wanamwongeza maji, kumfanyia vipimo na kumpatia dawa ya antibiotiki, kumpa dawa za kurutubisha zinazoitwa zinki.

"Wazazi au walezi wawe makini wakati wa kuandaa chakula cha watoto na wanapowapatia chakula hicho," alihadharisha.

Mtaalamu huyo wa afya alisema mtoto akipata shida hiyo, anapaswa kukimbizwa hospitalini kwa kuwa akicheleweshwa, anapoteza madini ya potassium mwilini na kuleta shida kwenye moyo baada ya miezi sita kupita.

Alitaja madhara mengine anayoweza kuyapata mtoto kuwa na shida ya figo kama amepoteza maji mengi.

Alifafanua kuwa watoto wengi wanapatwa na ugonjwa huo chini ya mwaka mmoja kwa kuwa wanakuwa wametoka kipindi cha kunyonya tu, wanahamia kuanza kula chakula.

Daktari huyo alisema wazazi au walezi hawashauriwi kutumia chupa au nyonyo kuwapa chakula kwa kuwa zinachangia watoto kuhara, ni muhimu mtoto anyweshwe kwa kikombe, chupa. Nyonyo ambazo hazioshwi vizuri ni chanzo cha magonjwa.

"Nyonyo zinakuwa hazijaoshwa vizuri kama zinakuwa hazijawekwa kwenye maji ya moto na namna ya kutunza ni tatizo kwa wazazi wengi," alisema.

Mkazi wa Babati, Neema Festo, alisema watoto wengi wanapatwa na ugonjwa huo kutokana na kucheza katika mazingira yenye uchafu.

Mkazi mwingine Godwin John, alisema wanajua watoto wakihara sana wanakuwa wanaota meno.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, ACP George Katabazi (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jana, wakati akiwaonyesha baadhi ya vifaa vinavyofungwa kwenye pikipiki vinavyotoa milipuko na mwanga mkali na kusababisha taharuki baada ya kuvikamata. **PICHA: JALIWASON JASSON**

MGOGORO ARDHI LOLIONDO

# Mahakama yasema tangazo la waziri ni batili

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha imetoa hukumu ya kesi ya wanavijiji wa Loliondo baada ya kujiridhisha tangazo la Waziri wa Maliasili na Utaliii alilolitoa kwa kutumia Tangazo la Serikali (GN) Na. 421 la Juni 17, 2022 kuhusu ardhi ya vijiji vya Loliondo kuwa Pori Tengefu la Pololeti, halikufuata taratibu za kisheria.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Joachim Tiganga.

Vilevile, mahakama hiyo imetupilia mbali hoja nyingine tisa za waleta maombi baada ya kuzipitia na kujiridhisha kuwa hazina ushahidi wa kutosha.

Katika hukumu hiyo, Jaji Tiganga alisema mahakama hiyo ilitoa muda kwa pande zote mbili kuwasilisha hoja zao. Baada ya kupitia hoja hizo ilijiridhisha tangazo hilo ni batili kwa kuwa waziri hakufuata sheria katika kutoa tangazo hilo. Jaji Tiganga alisema mahakama inashindwa kutoa uamuzi zaidi kwa kuwa tayari Rais alishatoa tangazo la kulipandisha hadhi pori hilo, hivyo tangazo la waziri halikuwa na nguvu tena.

"Mahakama haiwezi kutoa zuio. Mahakama pia haitamzuia Waziri wa Maliasili na Utalii kutoa uamuzi wa kutangaza pori hilo kuwa tengefu endapo atafuata utaratibu.

"Mahakama kwa kuzingatia kuwa Rais ndiye mwenye mamlaka ya kutangaza kupanda kwa hadhi ya Pori Tengefu kuwa Pori la Akiba, Tangazo la Serikali Na. 421, lishapita na hivyo yeyote anayepinga anaweza kukata rufani juu ya uamuzi wa Rais," alisema Jaji Tiganga.

Mawakili wa Jamhuri wanaosimamia kesi hiyo ni Ian Mbise na Mkama Msalama huku upande wa wajibu maombi ukiwakilishwa na Joseph Alais, Denis Moses, Yonas Masiaya na Joseph Oleshangay.



# Vizimba vya taka vyageuka kero

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

VIZIMBA 12 vilivyotengwa kwa ajili ya kuhifadhia taka kwa muda katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza, vimejaa na kuanza kumwaga uchafu katika mazingira ya mji huo.

Hali hiyo imesababisha kero kwa wakazi na wafanyabiashara mbalimbali wa maeneo husika kutokana na taka hizo kutokuondolewa kwa muda.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wananchi na wafanyabiashara katika mji huo walisema kutokuzolewa kwa taka hizo kwa wakati kunahatarisha afya zao hususani katika kipindi cha mvua.

**Tunaiomba serikali kuweka utaratibu maalumu kwa ajili ya kuzoa na kudhibiti mwenendo wa taka hizi...**

"Tunaiomba serikali kuweka utaratibu maalumu kwa ajili ya kuzoa na kudhibiti mwenendo wa taka hizi ambazo zimegeuka kero katika mazingira yetu ya biashara na kuishi pia kwani hali hii inasababisha tunakosa mpaka wateja," alisema Retisia Wilbert ambaye ni mama lishe.

Mtendaji wa Kata ya Nyatukala, Obokila Masukila, alisema vizimba vinajaa kutokana na utaratibu wa wananchi wote kusomba na kuweka taka zao katika vizimba hivyo hadi kufikia kumwaga chini, hivyo kuwataka kuweka utaratibu wa kuwa na vifaa vya kuhifadhia taka katika maeneo yao ili kuondoa adha ya kumwaga taka hizo katika maeneo yasiyo husika ili kuweka mji safi.

Ofisa Afya na Mazingira wa Halmashauri hiyo, Wilbert Muyumbu, alisema chanzo za taka hizo kutokuzolewa kwa muda mrefu ni kutokana na uhaba wa matrekta ya kuhamisha na kupeleka katika eneo maalumu. Alisema kwa sasa lipo moja ambalo linalazimika kuzungukia vizimba vyote 12.

Pia alisema ukosefu wa fedha kwa ajili ya kununua mafuta ya trekta hilo ni moja ya sababu kutokana na wananchi kutokuwa na mwamko katika kuchangia huduma ya uzoaji wa taka katika mazingira yao.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Sengerema, Cuthbert Midala, alisema kutokana na kero hiyo, atamwagiza Mkurugezi Mtendaji wa Halmashauri kuhakikisha anapitisha gari kwa ajili ya kuzoa taka sehemu zote zenye vizimba ili kuhakikisha mji wa Sengerema unakuwa katika hali ya usafi.




Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana (katikati), akitoka katika Gereza la Bariadi, Mkoa wa Simiyu juzi, baada ya kuzungumza na kutoa elimu ya sheria kwa wafungwa na mahabusu kupitia Kampeni ya Huduma Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayoendelea mkoani humo. Kulia ni Mkuu wa Gereza hilo, SSP George Mwasalyanga na (kushoto) ni Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Simon Simalenga. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waonywa kufuga wahamiaji haramu

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (pichani), amewataka wananchi wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, kuacha tabia ya kufuga wahamiaji haramu kwa kuwatumikisha kwenye mashamba ya tumbaku, hali ambayo ni hatari kiusalama.

Alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Bugela Kata ya Ulowa kwenye mkutano wa kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua.

Mndeme alisema wananchi kuishi na wahamiaji haramu ni hatari kiusalama na kuwataka wafuate utaratibu wa kuishi nao katika idara ya uhamiaji kwa kuwakatia vibali vya kuishi nchini.



"Moja ya kero ambazo nimezipokea hapa kwenye mkutano ni ukosefu wa ulinzi na usalama kutokana na wananchi kuibiwa fedha zao na watu ambao wanadaiwa kuwa wahamiaji haramu ambao wengine mnaishi nao na kuwatumikisha kwenye mashamba ya tumbaku," alisema Mndeme.

Aliliagiza Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji, kulifanyia kazi suala hilo na kuwaondoa wahamiaji wote haramu ambao wamekuwa wakifanya kazi kwenye mashamba ya tumbaku kwa kuishi nchini kinyume na utaratibu.

Kero hiyo iliibuliwa na mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Bugela, Malulu Njamba na kueleza kuwa ukosefu wa amani kijijini hapo unatokana na kuwapo wahamiaji haramu ambao wamekuwa wakiwaibia mali zao, zikiwamo fedha.

Akijibu kero zingine zikiwamo za ubovu wa miundombinu ya barabara, ukosefu maji, umeme, ujenzi wa maboma ya zahanati kutokamilika, alisema zaidi ya Sh. trilioni moja zimetolewa na Rais Samia Suluihu Hassan kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aidha, akiweka jiwe la msingi katika shule mpya ya sekondari Ngilimba iliyoko Ulowa Halmashauri ya Ushetu, Mndeme aliwataka wazazi kupeleke watoto wao shuleni ili wasome na kutimiza ndoto zao na hata kuja kuwa viongozi wa baadaye.

# Waomba huduma ya mama, mtoto

**Shaban Njia na Marco Maduhu,** KAHAMA

WAKAZI 39,908 wa Kata za Bulige, Kashishi na Kijiji cha Mwashimbayi Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuwasogezea karibu huduma ya mama na mtoto kwa kuwajengea kituo cha afya chenye uwezo wa kutoa huduma hizo.

Kuwapo kwa huduma hizo kutaondoa adha ya kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 15 kufuata kituo cha afya.

Kukosekana kwa huduma hizo karibu pamoja na zingine zikiwamo za upasuaji, wananchi hao wanalazimika kuzifuata katika kituo cha Afya Ngaya kilicho umbali wa zaidi ya kilometa 15 hali inayosababisha kinamama kujifungulia njiani na wakati mwingine nyumbani.

Aidha, wameomba serikali kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Bulige ambacho ujenzi wake ulianza Februari, mwaka huu, kwa gharama ya Sh. milioni 500 kwa kuanza kukamilisha jengo la wagonjwa wa nje (OPD), mama na mtoto na maabara ili huduma zianze kutolewa.


Walibainisha hayo juzi wakati Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alipotembelea ujenzi na kuweka jiwe la msingi katika Kituo cha Afya Bulige na kutaka ujenzi wake ukamilike ifikapo Novemba Mosi, mwaka huu na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mkazi wa kata hiyo, Mariam Lukaje, alisema zahanati iliyopo inaelemewa na kuhudumia wagonjwa kutoka kata ya Kashishi na vijiji jirani, hivyo kufanya baadhi ya huduma kuzipata Kituo cha Afya cha Bulige ambacho kiko umbali wa kilometa 15 huku wengine wakijifungulia njiani.

Alisema wanapopata mgonjwa nyakati za usiku kwa gharama ya pikipiki wanatozwa Sh. 20,000 na kwa gari ni Sh. 100,000 na wale wasio na uwezo wa kumudu gharama hizo, wanapoteza maisha kwa kukosa huduma au vichanga vyao kufia tumboni.

Awali, akitoa taarifa ya ujenzi, Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Bulige, Catherine Peter, alikiri zahanati hiyo kuelemewa na wagonjwa na kwa siku wanahudumia wagonjwa 80 kati ya hao wajawazito wanaojifungua ni 25 hadi 30 kwa siku na wale wanaohitaji huduma ya upasuaji wanapelekwa kituo cha afya Ngaya.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 21, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**KUTAPAKAA 'UNGA' MAJUMBANI... Baadhi ya dawa tiba zinalevya, kutibiwa duka la dawa majanga**



**Bodaboda, chanzo kipya cha magonjwa yasiyoambukiza kutapakaa kwa kasi nchini**

Ukurasa 12

# Dk. Samia azuru Lindi, Pwani akiacha darasa mazingira yao utajiri walioukalia

**Na Mwandishi Wetu**

MARA zote mazingira ni msamiati nyeti unayogusa uhai, nyendo za kijamii, uchumi hata afya. 'Mazingira ni Uhai', hilo si la kubisha.

Vilevile, kuna msamiati mwingine unaitwa 'Rais'. Wataalamu wa fani tofauti wakiwamo wanasosholojia na wanasheria, katika sura moja wanaiangalia kuwa nafsi, lakini katika mfumo wa utendaji wake anabeba sura ya kitaasisi, kuegemea maelekezo yake, pia sheria, sera na miongozo ya kitaifa na kimataifa.

Kulingana na mamlaka kubwa aliyo nayo rais, mara zote umma hutarajii utashi na majibu ya mahitaji yao.

Kuwapo mwingiliano wa mawili hayo, wakazi wa mikoa ya Kusini na Pwani ambako wiki hii wameneemeka kutembelewa na mkuu wa nchi, Dk. Samia Suluhu Hassan, walipata shauku na hamasa kubwa ya ugeni huo kwa ziara iliyoisha jana mchana, Rais na taasisi anayoisimamia pale Ikulu.

Katika moja ya mambo ambayo Rais Dk. Samia naye akawaonyesha wenyeji wake hao, ni kwamba katika kuiwekea nguvu zake katika uchumi kama taasisi ya kibinadamu, bado wako chini ya mazingira, ambayo ina tabia na kanuni "usipoyaheshimu, nayo hayatakuheshimu."

Dk. Samia akiendana na tukio la kuwekeza mradi wa kihistoria wa Bandari Kilwa, akatoa maboti ya mikopo nafuu kwa wakazi hao wa Kilwa mkoani Lindi na majirani zao wa Pwani.

Kwanza, akawaeleza inawasaidia kukabili pengo la kimazingira kwamba kulingana na hali iliyojitokeza katika mustakabali wa mazingira, samaki hawapatikani kirahisi katika ukanda huo, hali inayowashinikiza wavuvi kufika mbali katikati ya bahari.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza jambo na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, kuhusiana na boti za kisasa za uvuvi baada ya kuzindua ugawaji wa boti hizo, Kilwa Masoko mkoani Lindi. **PICHA: MTANDAO**

Vilevile, akataja kuwa ni nyenzo muhimu kusaidia Uchumi wa Buluu, unaotegemea mazingira, kinamama wazalishaji wa zao la mwani, nako sasa wanakuja juu katika ufukwe wa Kilwa.

Mazingira kuharibika, ni mwendo unaolazimisha haja ya kuwapo vifaa bora na vya kisasa kufuata samaki waliko, kama ambavyo wakikabidhiwa wavuvi juzi bandarini Kilwa.

Anayekabidhi Dk. Samia akawaachia salamu za matendo kwamba, lolote linaloenda kinyume na utunzaji mazingira, linamgusa hata mwenyeji maana kukosekana samaki ukanda wa ufukwe wa bahari unaacha magumu, hata ngazi ya kiuchumi.

Akiwa njiani kurejea wilayani Rufiji, Rais Dk. Samia akarejea hoja ya mustakabali wa thamani ya mazingira na uchumi, ambako akawakumbusha wakazi kubarikiwa kuwa na 'Bonde la Rufiji' ambalo lina thamani kubwa kwa maisha yao.

Maelezo ya mkuu huyo wa nchi kwa mkusanyiko uliosimama kumsalimia katika msafara wake kutoka mkoani Lindi, akiwa Ikiwiriri, akawataka kuwekeza katika kilimo cha mpunga kwenye Bonde la Mto Rufiji, ambako kuna thamani kubwa sana, akiwanong'oneza anatakiwa sana kwenye soko la kimataifa.

Kwa mujibu wa Rais Dk. Samia, ni kwamba kuna sehemu ya bonde hilo la Rufiji, ndiko kunapatikana mradi wa Mradi wa Umeme wa Mwalimu Nyerere na sehemu iliyobaki inaweza kutumiwa kwa busara, hata ikabadili maisha yao.

Rais anataja kinachofanywa na serikali, inalenga kuwekeza kwenye skimu za umwagiliaji mahali hapo, taifa linufaike na zao la mpunga na kwa mtazamo wa awali kiserikali, ni kuandaliwa hekta 3,000 za mashamba ya mpunga, akiwashauri wananchi nao 'kuchangamkia' fursa.

Hapo Dk. Samia, katika nafasi ya kipekee, anataja haja ya kushirikisha vijana kupitia mradi mpya katika Wizara ya Kilimo inayoitwa BBT (kama wa Dodoma), kwamba vijana wanakusanyika na kuzalisha mpunga.

Kimsingi, thamani ya Bonde la Rufiji, iko juu tangu zama zilizopita na ndio maana kukaundwa iliyokuwa Mamlaka ya Bonde la Mto Rufiji (RUBADA).

Ni katika kipindi hicho kukashuhudiwa mahali hapo kuna miradi mbalimbali ya uzalishaji chakula shambani, zikiwamo kutoka katika kampuni za Kikorea.

Mtazamo huo wa Kimazingira, kutoka Bonde hilo la Rufiji, lina uhusiano wa moja kwa moja na uzalishaji umeme wenye ukubwa uliotukuka katika ngazi ya Bara Afrika, katika Mradi wa Mwalimu Nyerere, ambao ni sehemu ya majukumu yake nyeti kuwezesha upatikanaji umeme kitaifa.

AFYA

# Bodaboda, ilivyo chanzo kipya cha magonjwa yasiyoambukiza kutapakaa kwa kasi nchini

**Na Mwandishi Wetu**

MTINDO wa kutumia bodaboda kwa ajili ya usafiri wa hapa na pale katika maeneo ya mijini na vijijini, umetajwa kuchangia kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza nchini na kusababisha watu wengi kubweteka na kuacha kutembea.

Changamoto hiyo ni miongoni mwa zilizotajwa kuchangia kuendelea kuongezeka kwa magonjwa hayo nchini kwa kasi ikilinganishwa na miaka ya nyuma kabla ya usafiri huo kuanza.

Sababu nyingine zilizotajwa kuchangia kuongezeka kwa magonjwa hayo nchini ni jamii kutozingatia ulaji vyakula kwa afya, kutofanya mazoezi na unywaji wa pombe kupita kiasi.

Hayo yamebainika wakati Shirikisho la Vyama vya Magonjwa yasiyoambukiza nchini (TANCDA) lilipoandaa kikao kazi baina yake, wadau na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini.

Mgeni rasmi, Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, akawataka wahariri kutumia kalamu zao kupaza sauti kwa lengo la kuelimisha jamii namna ya kudhibiti magonjwa hayo nchini.

Hatua hiyo ya kuandaa kikao hicho imekuja baada ya vyama hivyo kufanya utafiti na kubaini, magonjwa hayo yanazidi kuongezeka kwa kasi nchini, hata kuwa tishio kwa nguvu kazi ya taifa na familia kubaki maskini, anayeugua na wanaouguza pia kuchangia vifo.

Wataalamu wa afya walibainisha kuwa, asilimia 50 ya wagonjwa wa kisukari ambao ni miongoni mwa magonjwa hayo yasiyoambukizwa, inaweza kupona, iwapo mgonjwa atagundulika mapema.

Dk. Heri Marwa, Mkurugenzi wa PharmAccess, anaonya kwamba, hatua isipochukuliwa dhidi ya magonjwa hayo, siku za baadaye yatakuwa janga kwa taifa na familia.

"Magonjwa yasiyoambukiza ni mapambano yetu wenyewe kwa wenyewe, presha (shinikizo la damu) gharama kwa mwezi ni kati ya Sh. 40,000 hadi 60,000 kwa mwezi, hapo unaongelea robo ya mshahara wa mtu kwa mwezi kwa ajili ya gharama za kununulia dawa," anafafanua.

Mbali na gharama hizo za dawa, Dk. Marwa anasema pia, mgonjwa na ndugu wamekuwa wakipoteza muda kwenda hospitalini kufuatilia matibabu na dawa.

"Mgonjwa akipata matatizo, familia inaingia katika umaskini, familia moja, baba aliamua kuuza nyumba na gari na miezi mitatu baadaye akafariki dunia," anasimulia mtaalamu Dk. Marwa.

Anasema magonjwa hayo, mbali ya kuisababisha hasara serikali kwa kupoteza nguvu kazi, pia yanaathiri uchumi na afya za Watanzania.

"Wahariri tunaomba mhamasishe waandishi wa habari kufichua habari za wagonjwa wa magonjwa



Waendesha bodaboda, wakiwa na abiria zao. **PICHA: MTANDAO**

haya katika jamii.

Anabainisha kuwa, TCD (Chama Wagonjwa wa Kisukari Tanzania) kinawezesha waandishi kwenda kuandika habari kuhusiana na magonjwa hayo katika jamii ambayo chanzo chake kikuu ni vyakula ambavyo vinaliwa, vinywaji vyenye sukari kama juisi na pombe.

"Kuna haja ya serikali kutunga sheria ya kudhibiti vitu hivyo na wahariri kupaza sauti ya kukekemea," anasema Dk. Marwa.

Kampuni hiyo yenye makao yake nchini Uholanzi inafanya kazi zake Tanzania Bara na Zanzibar, ya kupambana na magonjwa hayo nchini.

Mwenyekiti wa TANCDA na Chama cha Kisukari Tanzania (TDA), Profesa Swai anasema TDA kilianzishwa nchini mwaka 1985, kuwawezesha wagonjwa kupata msaada wa matibabu.

Programu Meneja wa NCA, Veleria Milinga anataja viashiria vya magonjwa hayo kuwa ni utandawazi, ukuaji wa miji, ongezeko la watu hasa wenye umri mkubwa na urithi wa vinasaba.

Anasema viashiria vinavyoweza kubadili hali ni ulaji wa mboga za majani na matunda, matumizi ya pombe, tumbaku, kuacha tabia bwete na uzito.

Veleria anasema kila mwaka watu 40,464 wamegundulika kuwa na ugonjwa wa saratani, kati ya hao, asilimia 25.3 wana saratani ya mlango wa uzazi, 9.9 matiti na 8.5 tezi dume.

Anasema kuwa kati ya watu hao wanaogundulika kuwa na ugonjwa huo, 26,945 hufa kila mwaka nchini.

### NHIF & MUHIMBILI

Mkurugenzi wa Huduma za Matibabu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Raymond Mwenesano, anasema serikali inatumia fedha nyingi kutibu magonjwa hayo kwa wanachama wa mfuko huo, wategemezi wao na wasio wanachama.

Mwenesengo anasema kwa mwaka wa fedha wa 2021/22, mfuko huo ulitumia shilingi bilioni 35 kutibu ugonjwa wa kisukari kwa wanachama wake.

"Mfuko unaelewa kwa sababu idadi kubwa ya wananchi hawawezi kumudu gharama kubwa za vipimo na dawa," anasema.

Hata hivyo, anasema bado mfuko unategemea wadau wa maendeleo katika afya, kwa ajili ya kugharamia huduma za matibabu kwa wanachama wake na wategemezi wao.

Dk. Elisha Osati kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), anasema asilimia 70 ya magonjwa ya figo yanachangiwa na kisukari na shinikizo la damu.

"Tatizo ni kubwa, kwa sababu wagonjwa wanafika hospitalini (serikali) wakiwa katika hatua mbaya, kwa sababu wanaanza kwa kwenda kutibiwa kwenye hospitalini za binafsi na waganga wa kienyeji," anasema.

Anaongeza kuwa wanapofika Muhimbili na kulazwa, gharama za matibabu ni kubwa na wengi wao wanashindwa kumudu," anasema.

Anatoa mfano wa matibabu ya figo, kuwa gharama zake kuwa ni kubwa na wagonjwa wengi wanaolazwa Muhimbili hawana uwezo wa kulipa gharama za matibabu.

Akizungumzia kuhusu ugonjwa wa ini, anasema wanaokunywa pombe kupita kiasi, wako hatarini kukumbwa na ugonjwa huo.

### MWAKILISHI WHO

Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Alphoncina Nanai anasema kati ya vifo milioni 41 vilivyotokea duniani mwaka 2008, milioni 31.4 vilisababishwa na magonjwa hayo yasiyo ya kuambukizwa. Vifo hivyo ni sawa na asilimia 74.

Alphoncina anasema, vifo hivyo viliwakumba watu milioni 17 wenye umri chini ya miaka 70.

"Wengi ni kutoka kwenye nchi kama zetu (Afrika)," anasema, akiwa na ufafanuzi, magonjwa ya shinikizo la damu na mengine yanayoshika mfumo wa damu yanasababishwa na magonjwa hayo yasiyo ya kuambukiza.

Hata hivyo, anasisitiza kuwa WHO imepania kupunguza vifo vya magonjwa hayo hadi kufikia moja ya tatu mwaka 2030.

"Tunaona umuhimu wa kuzuia haya magonjwa, yule anayeumwa leo yuko wapi, huyu ana maana kwetu... huyu anaanza kuwa na presha, siku nyingi anakuwa hajui baadaye anaanza kuumwa sukari, inaua macho, figo baadaye anapata 'stroke'," anasema.

Mkuu huyo wa WHO anaongeza: "Siku anaposikia hiyo hali anakwenda hospitali na kugundulika kuwa na magonjwa hayo."

### MKUU WA NCD

Mkurugenzi wa Magonjwa yasiyoambukizwa wa NCD kutoka Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, anatoa mfano kuwa mwaka 1960, magonjwa hayo yalikuwa tatizo kubwa nchini Finland, ikilinganishwa na nchi nyingine duniani.

"Walichofanya walianzisha mkakati wa namna ya kukabiliana na vyakula ambavyo havifai na kuchangia kuibuka kwa magonjwa hayo," anasema.

Dk. Ubuguyu anasema, kampeni ya kupinga ulaji wa vyakula hivyo na unywaji pombe kupita kiasi, iliendeshwa na waandishi wa habari.

Anasema kampeni hiyo ya kukabiliana na magonjwa hayo ambayo yalionyesha kuathiri wanaume kwa kiasi kikubwa ilifanikiwa kutokana na raia wa nchi hiyo kubadili ulaji wao wa vyakula na afya zao zikabadilika na kuwa salama.

Anasema kwa nchini walifanya utafiti na kubaini kuwa magonjwa hayo yanachangiwa na jamii kutofanya mazoezi.

Anasema utafiti unaonyesha kuwa mwaka 2012, idadi kubwa ya watu nchini hawafanyi mazoezi kwa hiyari kutokana na kutofahamu umuhimu wake na uvivu.

Anafafanua kuwa kiwango kinachotakiwa kufanya mazoezi ni asilimia 33 ili kuweza kukabiliana na magonjwa hayo.

Vilevile anasema kutembea umbali fulani kwenda kupanda daladala kwa ajili ya kusafiri maeneo mbalimbali ni njia mojawapo ya kuzuia magonjwa hayo kwa mwanadamu na kilimo.

"Tangu kuanza kwa usafiri wa pikipiki, watu wamekuwa wavivu kutembea unakuta hapa na hapa anaita pikipiki inakuja kumchukua mlangoni nyumbani kwake na kumpeleka hadi kwenye kituo cha daladala anaingia kwenye basi na kuishia," anasema na kuongeza kuwa:

"Anapoteremka kwenye daladala anachukua tena pikipiki na kwenda nayo hadi anakotaka kwenda iwe ofisini au kwingineko."

### KUTOKA TAMISEMI

James Kengia kutoka Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anasema uelimisaji katika jamii na utambuzi katika vituo vya afya dhidi ya magonjwa hayo unatakiwa kufanyika.

Kengia anasema, iwapo watu watajitokeza katika vituo vya afya na kupima afya mapema, wakigundulika kuwa na magonjwa hayo watapatiwa matibabu na kupona.

AFYA

# Ijue operesheni maalum ilivyopunguza mimba, ndoa za utotoni Rukwa, Katavi

## • 'Jambo halieleweki' watoto wanaripoti wenyewe…



Wanafunzi katika mjumuiko wao kitaaluma. Ni sehemu wanakohitaji utetezi na usalama zaidi. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Zuwena Shame, aliyekuwa SUMBAWANGA**

KATIKA jamii ndani na nje ya nchi, kuna kilio kinacholalamikiwa kuwapo vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, vikiharibu msingi imara wanayoihitaji, ili kuwa na afya na maisha bora yenye tija.

Ni ukatili unaotajwa kusigana na haki, pia msingi ya watoto kuishi salama. Serikali na taasisi mbalimbali nazo zimekuwa mstari wa mbele kupigania kumlinda mtoto dhidi ya ukatili wa namna zote.

Wakati Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inaelekeza utoaji huduma za ulinzi na ustawi wa mtoto, Plan International, imo katika mashirika nchini yanayoweka mikakati kupinga na kukemea ukatili kwa watoto.

Hiyo ni kupitia Mradi wa Kupinga Mimba na Ndoa za Utotoni Mkoa wa Rukwa, unadhamiria kuinua wasichana kupata haki ya msingi ya elimu na kupinga aina zote za ukatili, ikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

Utafiti ulioshirikisha Nipashe na Shirika Plan International katika wilaya za Kalambo, Nkasi na Sumbawanga Vijijini mkoani Rukwa, hivi karibuni unaonyesha vitendo vya ukatili vimepungua.

Walidadisiwa maofisa elimu walimu, viongozi wa dini, wahamasishaji rika na viongozi wa serikali, wasichana na wanakamati za vijiji, ambao mradi unatekelezwa katika kata 10, kati ya 27, zenye mradi huo, hata kupata picha kamili.

Jumanne Wilson, Mwalimu wa Malezi na Afya kutoka Shule ya Msingi Milepa, katika Kata ya Milepa, wilayani Sumbawanga Mkoa wa Rukwa, anasema ukatili kwa watoto kuanzia shuleni hadi mitaani sasa umepungua.

Anafafanu sababu ni kwamba wanafunzi wengi sasa wana uelewa kuhusu elimu ya ukatili, pia wapo wanaoripoti pindi vitendo hivyo vinapotokea.

Wilson anabainisha, awali vitendo hivyo vilikuwa vingi na havikuripotiwa, hata sasa vimepungua kufikia idadi vitatu mwaka jana, huku mwaka huu kikiwa kimoja pekee na haikufanyika katika mazingira ya shule.

"Kupitia Mradi wa Kupinga Mimba na Ndoa za Utotoni Mkoa wa Rukwa, uelewa wa jinsi ya kuripoti vitendo vya ukatili ni mkubwa," anasema mwalimu huyo.

"Wanafunzi wanajua njia ya kuripoti ngazi kwa ngazi na wana uthubutu. Shuleni tuna masanduku ya maoni, hufunguliwa kila wiki na wengine huripoti kwa walimu moja kwa moja" anaendelea Mwalimu Wilson.

Anatoa mfano kesi za ukatili zilizotokea mitaani na kuripotiwa shuleni, ni mwanafunzi kupigwa na mama yake wa kambo na nyingine alikuwa hapewi mahitaji yake muhimu ya msingi, kama vifaa vya shule na akatoroka kwao.

Anasema, mafanikio hayo ni zao la ushirikiano wa karibu kati ya mradi, serikali na Umoja wa Walimu na Wazazi (UWAWA), wanaohakikisha wanafunzi wanapata elimu na kuendelea na masomo yao, hata wakafaulu.

> **"Kupitia Mradi wa Kupinga Mimba na Ndoa za Utotoni Mkoa wa Rukwa, uelewa wa jinsi ya kuripoti vitendo vya ukatili ni mkubwa," anasema mwalimu huyo.**

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Milepa na Mwenyekiti wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), Desderi Raphaeli, anasema kipindi cha awali kulikuwapo na ukatili.

Hapo anajumuisha namna watoto na kinamama kwenye kata hiyo, ambao watoto waliacha shule na kufanya kazi hatarishi kama kuvua samaki Ziwa Rukwa na kuchunga mifugo.

Kupitia Shirika la Plan International, anataka pia kukawapo jitihada za Kamati ya Ulinzi na Usalama dhidi ya Ukatili wa Watoto, wakafanikiwa kuokoa watoto wanane katika ajira hizo, wakarudi shuleni.

"Tuliweza kushirikiana na Plan na kugundua sababu ya watoto hao kuajiriwa, ni hali duni ya kiuchumi kwa wazazi na walezi. Hivyo, tukaanzisha programu ya chakula na kuwawezesha wazazi kiuchumi," anasema Desideri.

Anatoa mifano ya matukio ya kuozwa kwa mwanafunzi wa darasa la saba, hivyo Kamati ya Ulinzi na Usalama, ikaingilia kati na kuvunja ndoa, watuhumiwa wakafikishwa mbele ya sheria, huku msichana shuleni alifaulu na kuendelea na sekondari.

Mwenyekiti wa Klabu ya Wazazi Kata ya Matai A, Wilaya ya Sumbawanga, Isaac Sawala, anasema kuna mafanikio makubwa kwenye kukabili ukatili wa watoto, kwani vitendo hivyo vinaripotiwa na kufanyiwa kazi katika ngazi tofauti.

Pia anasema kabla ya mradi na elimu kuenea, vitendo vya ukatili vilishamiri na kulikuwapo kesi tano, mojawapo ikihusu wazazi kushindwa kumpatia mtoto mahitaji muhimu ya shule, hata kumfanya mtoto akashindwa kusoma.

Inaelezwa, kutokana na uelewa wa mtoto huyo akaweza kuripoti tukio kwenye klabu ya wazazi na akapatiwa msaada.

Anasema, kwa sasa elimu ya ukatili imesaidia sana kwani kupitia klabu za wazazi, baadhi ya mila na desturi potofu ndani ya jamii kama kuongea na mtoto kuhusu masuala ya afya ya uzazi ni huru.

Mwelimisha Rika, Neema Kasomo kutoka Kata ya Kipundu-Wilaya ya Nkasi, anafafanua kwamba, elimu ya ukatili kwa sasa imegeuka mkombozi katika familia nyingi, kukiwapo uwazi wa wazazi kuzungumzia suala hilo.

Kasomo anakiri wazazi wanajua madhara ya ukatili kwa mtoto, mojawapo ni kwa wasichana kuwakimbia wazazi na mwisho wanapata mimba katika umri mdogo.

Mwelimisha Rika, Janeth Kuchankwa, kutoka kijiji cha Mashete, wilayani Nkasi anasema baadhi ya mila na desturi wilayani humo zinachangia ukatili kwa watoto, mfano msichana kutopata elimu na anaolewa au kusaidia kazi za nyumbani.

Kuchankwa anasema, kwa kushirikiana na Plan International, pia wadau mbalimbali kutoa elimu kwa wazazi kupitia mikutano ya kijiji na kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa, ili kuwawezesha wazazi kiuchumi na kuwapatia watoto mahitaji ya shule.

### ASKOFU KKKT

Askofu Ambele Mwaipopo kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Ziwa Tanganyika, mikoa ya Katavi na Rukwa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maridhiano ya Amani kwa viongozi wa dini Rukwa, anasema vitendo vya ukatili wa aina yoyote ni vya kukemewa, kwani vinaharibu ustawi wa jamii.

Anataja baadhi ya mila na desturi zimechangia vitendo vya ukatili, kwani mtoto anapofanyiwa hayo, wazazi humalizana na mhusika ili kuficha maovu hayo, wakidai kulinda heshima ya familia bila yac kujali athari anazopata mtoto.

Askofu Mwaipopo, anashauri ni vyema viongozi wa dini wakatumia majukwaa yao ipasavyo wakati wa ibada, wakahubiri kila mara, namna ya kutoa elimu sahihi, wakikemea mabaya hayo.

### MRADI MIMBA&NDOA

Meneja wa Mradi wa Kupinga Mimba na Ndoa za Utotoni Mkoa wa Rukwa, Kisasu Sikalwanda, anasema bado vitendo vya ukatili vinaendelea kuwa changamoto mkoani Rukwa.

"Pia kufanyike kampeni kubwa ya kuendelea kutoa elimu katika ngazi za jamii, kimkoa na hata kitaifa kuelimisha kuhusu madhara ya ukatili kwa watoto vilevile kuwahusisha watu muhimu katika jamii, vijana wenyewe, watu maarufu na vyombo vya habari kuhamasisha ujumbe chanya na mabadiliko ya tabia," anasema Sikalwanda.

AFYA

KUTAPAKAA 'UNGA' MAJUMBANI…

# Baadhi ya dawa tiba zinalevya, kutibiwa duka la dawa majanga



Hospitali ya Wilaya ya Longido ikiwa katika hatua ya ujenzi, itakomboa jamii hiyo kutegemea zahanati na vituo vya afya hata maduka ya dawa yanayotumiwa kwa matibabu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Zanura Mollel, ARUSHA**

DAWA Tiba ni vitu au utaratibu unaotumiwa kutibu, kuzuia au kupunguza dalili za magonjwa na matatizo ya kiafya kwa watu na wanyama.

Dawa hizo zenye asili ya kulevya inaweza kuleta athari za ama kulevya au utegemezi wa kimwili na kiakili kwa mtumiaji.

Mara nyingi dawa hizo zina viungo vya kemikali vinayoweza kusababisha hisia za raha au usingizi na hivyo husababisha mtumiaji kuhitaji dawa mara kwa mara.

Ingawa zinatumika kwa madhumuni ya matibabu, dawa tiba zenye asili ya kulevya zinahitaji kutumiwa kwa tahadhari kubwa na chini ya usimamizi wa kitaalamu, matumizi yasiyo sahihi huwa na kawaida ya kusababisha madhara kwa afya ya mtumiaji, ikiwamo utegemezi, kudhuru viungo vya mwili au hata kifo kuchangia.

Dawa hizo zinaweza kuchepushwa na kutumika kama za kulevya au kuchanganywa na dawa za kulevya. Hivyo kutumika bila ya kufuata ushauri wa daktari, hata kumletea mtumiaji uraibu.

### KULIVYO MPAKANI

Akizungumza na Nipashe, famasia wa Wilaya ya Longido Mkoa wa Arusha, Godlove Moshi, anasema uchepushwaji dawa tiba kutoka nchi jirani kuingia nchini, bado ipo na serikali inafuatilia kwa njia mbalimbali kudhibiti mianya yake inayotumiwa na wananchi waliokosa uzalendo.

Anasema, katika ukaguzi walioufanya walibaini duka za vyakula za mpakani kuonekana kuuza dawa tiba, ambako kunakijiji (jina tunalo), kulikuwapo duka la dawa zaidi ya miaka mitatu kinyume na taratibu na ikabainika kuwapo dawa tiba zenye asili ya kulevya.

Anataja athari za matumizi ya dawa hizo, bila ya ushauri wa daktari, ni pamoja na kusababisha tatizo kwenye ini kushindwa kufanya kazi, figo na maradhi ya kansa.

Moshi anasema, dawa hizo zinasababisha madhara makubwa, yakiwamo muwasho mwilini hadi vidonda, kunyonyoka nywele kichwani na maudhi kama vile kutapika, kuharisha na usingizi mzito.

Moshi anataja duka hilo la dawa haziruhusiwi kutoa dawa kwa mgonjwa bila ya cheti cha daktari, hawaruhusiwi kuchoma sindano na anataja katika msako wao walibaini kuna maduka yanazalisha wanawake, kutibu na kusafisha vidonda kinyume na taratibu, hata wakachukua hatua ya kuwapa elimu na onyo kali.

Hata hivyo, inaelezwa wilaya Longido, ipo mpakani, hata kuhitajika wananchi wasipokuwa makini, wanaweza kuuziwa dawa ambazo si salama.

"Dawa nyingi kutoka nchi jirani zipo kwenye makopo, huwezi kuona muda wa uzalishaji na mwisho wa matumizi kutokana na kufutika kwa maandishi, tofauti na hizi zinazoingizwa kwa kufuata taratibu zinazoonekana kuwa kwenye tembe," anafafanua Moshi.

Anasema, dawa tiba zinazotajwa zipo za asili za kulevya, hata katika vituo vya afya hutolewa kwa kufuata taratibu, pia kuna ukaguzi wa kujiridhisha kama zimetumika vyema na huwaruhusiwi kutupa chupa baada ya matumizi, hadi wakaguzi watakapojiridhisha.

Zinatajwa ni dawa zinazotumika na kwenye upasuaji, kwa wenye maumivu makali mfano wagonjwa wa kansa, baadhi hutumika kwa ajili ya usingizi kumsaidia ili mgonjwa aweze kufanyiwa upasuaji mkubwa mfano upasuaji wa sehemu za kichwa.

### KIMATAIFA

Ripoti ya Dunia ya Mwaka 2022, inaonyesha ukamataji dawa tiba zenye asili ya kulevya ulipungua kwa mwaka 2020, tofauti na ilivyokuwa awali.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa ongezeko la matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya, ilihusisha zaidi matumizi dawa kutoka Amerika Kaskazini, hata imeongeza vifo kuliko ilivyoshuhudiwa wakati wa janga la UVIKO-19.

Barani Afrika, ripoti inataja kuwapo dalili za kuongezeka matumizi yasiyo na matibabu, hasa kwa Afrika Kaskazini na Afrika Magharibi, vilevile matumizi hayo yalionekana kuongezeka katika nchi za Mashariki ya Kati na Kusini Magharibi mwa Asia.

### UKAGUZI NCHINI

Inaelezwa, kuna ukaguzi uliofanyika nchini kudhibiti dawa tiba zenye asili ya kulevya mwaka 2022, yakihusisha maduka ya dawa ya binadamu katika mikoa ya Geita, Mwanza, Arusha, Dar es Salaam, Shinyanga na Manyara.

Vilevile, kunatajwa kufanyika ukaguzi huo kwenye vituo saba vya Forodha katika mipaka ya Namanga, Kilambo, Hororo, Mtambaswala, Mkenda, Kasumulo na Tunduma na kwenye kampuni za usafirishaji na vifurushi vinavyopitisha mizigo katika kiwanja cha ndege KIA, Kilimanjaro na Shirika la Posta Dar es Salaam.

Moshi anataja kubainika uingizaji haramu wa dawa tiba zenye asili ya kulevya zikitokea katika nchi jirani.

Vilevile, anaeleza kukosekana nyaraka mbalimbali kwa baadhi ya maduka ya dawa kionyesha uhalali wa dawa hizo kuingizwa nchini.

### MADUKA YA DAWA

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe, unabaini maduka ya dawa za binadamu yanayouza au kutoa dawa kwa watu bila ya kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za miongozo ya Wizara ya Afya, ikiwamo kutoa dawa kwa mgonjwa aliyethibitishwa na daktari anahitajika kutumia dawa hizo.

Pia kuna uuzwaji bomba za sindano kienyeji hasa kwa wateja vijana.

### ALIYEDHURIWA AFUNGUKA

Esther Mkombozi, Mkazi wa Kimandolu jijini Arusha, ana simulizi ya kudhuriwa na huduma ya duka la dawa hata kupata ulemavu wa kudumu.

Anasimulia siku hiyo akiwa Arusha aliamka anajiskia vibaya na kufikiri yawezekana kwenye dalili za ugonjwa wa UTI, akaanza safari kuelekea duka la dawa za binadamu, baada ya kufika alifanyiwa vipimo na kuthibika ana maambukizi ya maradhi hayo. Mmiliki wa duka alimshauri kuanza dozi ya sindano kudhibiti hadi kutokomeza ugonjwa huo.

Anaeleza kwamba, akachomwa sindano kwenye mkono na haikuchukua muda mrefu akaanza kupata maumivu makali sana, hata akaamua kurejea kwenye duka hilo, akakuta kumefungwa.

Esther anasema, akalazimika kurejea nyumbani na siku ya tatu akaenda dukani ambako akamkuta mtoto wa mwenye duka, aliyempatia dawa ambayo haikumsaidia.

Hapo akafunga safari hadi kwenye duka lingine, akaelezwa dawa ni sahihi aliyokuchoma, ila hakupaswa kukuchomwa mkononi, kwamba inachomwa kwenye nyama (makalio)na si kwenye mshipa.

Akarejea nyumbani na maumivu makali zaidi, majirani wakampeleka kwenye duka lingine la dawa, baada ya kumuona ana hali mbaya. Huyo alikataa kumhudumia na akamshauri aende kwenye kituo cha afya. Hapo ndio safari ya kuelekea Kaloleni Hospitali ikatimia, ambako akapatiwa dawa za vidonge kwa siku tatu, hakuona mafanikio.

Mama huyo anasumulia Kaloleni wakamshauri aende kwenye Hospitali ya Rufani Mkoa wa Arusha, Mount Meru. Huko akapokewa na kuchomwa sindano iliyomsaidia kuondoa uvimbe mkononi, ila kulibaki rangi nyeusi. Pia, akampatiwa dawa za kutumia siku 20.

Baada ya dawa kuisha, anasema akarejea Mount Meru Hospitali, alikopatiwa dawa nyingine na baada ya kuzimaliza, akarejea kupata matibabu tena.

Madaktari wakamshauri, kutokana na hali ya mkono 'kupoteza mawasiliano' katika eneo lililojeruhiwa, hivyo ni vyema vidole hivyo vingeondolewa, kwani hakuwa anahisi chochote katika eneo hilo, yaani vidole vilikufa ganzi.

Sasa kilio chake ni umma kwenda kutafuta tiba penye vituo vya afya na si kwenye maduka ya dawa kupata mwongozo wa kidaktari, kinyume chake wanaangukia mikasa kama yake

Dk. Aman Kiru w a Kitengo cha Upasuaji, Hospitali ya Rufani Mountmeru, anakiri mkasa huo wa kidole cha mgonjwa wao kuharibika.

Sasa anawasisitizia wananchi pindi wanapopata changamoto au kuhisi kutokuwa sawa kiafya, kwenda katika vituo vya afya kwa matibabu na ushauri zaidi, kuacha kukimbilia huduma hiyo kwenye maduka ya dawa.

### SHERIA ILIVYO

Inatajwa, dawa hizo zinadhibitiwa kwa Sheria ya Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2015 na marekebisho yake ya Mwaka, 2017.

Ni sheria inayokataza kumiliki, kusafirisha, kununua, kuuza na kutengeneza dawa hizo kinyume na sheria.

Marufuku hiyio inagusa kuuza, kusambaza au kupata dawa tiba zenye asili ya kulevya, bila ya ruhusa ya kina mamlaka na utaalamu wa kidaktari.

Ni kosa ambalo lisilo na dhamana na adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni 50 au kifungo kisichopungua miaka 30 au adhabu zote mbili kwa pamoja.



# 220 wanaswa tuhuma za kumiliki silaha kinyemela

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi nchini limekamata watu 220 kwa kosa la kumiliki silaha kinyume cha sheria, huku 17 kati yao wakikamatwa kwa kosa la kumiliki risasi.

Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti na Usajili wa Silaha wa jeshi hilo, Kamishna Msaidizi Bertha Mlay, alibainisha hayo juzi jijini hapa wakati wa kikao cha Mtandao wa Polisi Wanawake Tanzania na viongozi wa makundi ya wanawake Mkoa wa Dodoma.

Alibainisha kuwa watu hao walikamatwa baada ya kukamilika kwa muda wa kuwasalimisha silaha kwa hiari Septemba mwaka jana.

Alisema uzagaaji wa silaha ndogo na nyepesi kwa jamii ni moja ya matatizo yanaloleta madhara kwa jamii, ndiyo maana jeshi limekuwa likikemea tabia hiyo na kutoa muda wa watu kurejesha silaha kwa hiari.

Alisema kila mwaka mwezi Septemba huwa ni mwezi wa msamaha wa kusalimisha silaha zinazomilikiwa kinyume cha sheria na baada ya muda huo, jeshi huanza kukamata wanaomiliki silaha hizo kinyume cha sheria.

Kamishna Msaidizi Bertha alisema kazi hiyo ilitakiwa kukamilika Septemba 30, lakini imeongezwa muda hadi Oktoba 31 mwaka huu, hivyo watu watumie muda huo kikamilifu.

Alisema kuwa silaha ina faida ikitumika vyema kwa kazi iliyokusudiwa na wakati mwafaka ila zikitumika kiholela na kinyume cha ilivyokusudiwa inaleta madhara. Sheria ya Udhibiti na Usajili wa Silaha ya Mwaka 2015 na kanuni zake za mwaka 2016, inaruhusu mtu binafsi na kampuni kumilikishwa silaha, matumizi yaliyoainishwa kwenye sheria hiyo ni kujilinda binafsi, kulinda mazao na kulinda wanyama na kuzitumia katika mashindano ya kulenga shabaha.

Alisema madhara ya uzagaaji wa silaha ni kuongeza uhalifu wa mauaji, uporaji mali, ujangili, ugaidi, wizi wa mifugo na uharamia baharini.

Mkuu wa Mtandao wa Polisi Wanawake Tanzania, Kamishna Msaidizi Eva Stesheni, alisema madhara ya uzagaaji silaha ni makubwa, hivyo ni wajibu wa kila anayemiliki silaha kinyume cha utaratibu kuzisalimisha.

# Mradi wazinduliwa kuwainua wanawake kiuchumi, uongozi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Maendeleo ya Jamii la TUSONGE limezindua mradi wa uongozi na haki za kiuchumi kwa wanawake katika Mkoa wa Singida, ukilenga kuondoa mfumo dume ambao umekuwa kikwazo kwa wanawake kushiriki masuala ya uongozi na haki za kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TUSONGE, Aginatha Rutazaa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa mradi huo unalenga kuleta mabadiliko na kuongeza uelewa wa jamii kwa wanawake kupambana na mifumo dume, kandamizi na ubaguzi ambayo haiheshimu ushiriki wao katika uamuzi hasa kiuchumi.

"Kazi iliyofanyika katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na sasa Mkoa wa Singida, kilio kikubwa ni ukiukwaji wa haki za wanawake ubaguzi, ukandamizaji na kuchechemua matukio, hali inayotokana na mila na desturi. Kwahiyo, njia pekee kuondoa matatizo hayo ni kuwapa wananchi elimu," alisema.

**viongozi katika maeneo ambako mradi wa uongozi na haki za uchumi kwa wanawake utafanya kazi watoe ushirikiano kwa shirika hilo ili malengo yaliyowekwa yafikiwe.**

Rutazaa alisema wanawake wakijumuishwa katika uamuzi kuanzia ngazi za chini, itasaidia kuleta sera zenye kuheshimu usawa wa kijinsia katika jamii.

"Serikali za mitaa ndiko chimbuko la mifumo dume na kandamizi ambayo inatokana na mila na desturi. Shirika litafanya kila jitihada kupambana na changamoto hiyo ili kuwe na usawa na idadi kubwa ya wanawake washiriki katika uongozi," alisema.

Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Singida anayeshughulikia Mipango na Uratibu, Romwald Mwendi, alisema kuwa ili kuondokana na mifumo dume inayokwamisha wanawake kufikia malengo kila mmoja ahakikishe anakubali mabadiliko.

Alisema viongozi katika maeneo ambako mradi wa uongozi na haki za uchumi kwa wanawake utafanya kazi watoe ushirikiano kwa shirika hilo ili malengo yaliyowekwa yafikiwe.

Mwensi alitoa wito kwa taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali kufanya kazi kwa uwazi ili serikali iwe inafahamu kila kinachofanyika kwa kuwa kunapokuwa na usiri kunasabisha serikali kuwa na shaka na mashirika hayo.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Mkoa wa Singida, Boniface Kitiku na Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Wilaya ya Ikungi, Neema Gwau, waliziomba taasisi na mashirika yasiyokuwa ya serikali kuwasaidia kuwapa elimu ili wawe na uelewa utakaowasaidia kupambana na tatizo la mfumo dume.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mbolea ya Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, akiangalia chakula cha ng'ombe alipotembelea shamba la Kampuni ya Asas Dairies, baada ya kuzindua aina saba za bidhaa mpya za lishe ya mifugo za Yara, Iringa Mjini juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yataka waandishi habari kulinda maslahi ya taifa

**Paul Mabeja na Gloria Maganza,** DODOMA

JESHI la Polisi limewataka waandishi wa habari nchini kuwa mstari wa mbele kulinda na kukuza maslahi mapana ya taifa wakati wote wanapotekeleza majukumu yao.

Msemaji wa Jeshi hilo, David Misime, alitoa rai hiyo juzi jijini hapa alipofungua mdahalo wa kitaifa kuhusu ulinzi na usalama kwa waandishi wa habari ulioandaliwa na Umoja wa Vyama vya Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC).

Misime alisema kazi kubwa ya jeshi hilo ni kulinda raia na mali zake, pia kuhakikisha usalama wa polisi, waandishi na jamii kwa ujumla inakuwa salama.

"Kazi ya waandishi wa habari ni muhimu sana na wakishirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa sahihi zenye kulinda amani ya nchi na kulinda maslahi mapana ya nchi ni wazi kila mmoja atakuwa salama na hapatakuwapo na malalamiko yoyote.

"Waandishi mnatakiwa kuandika habari ambazo zitakuwa na uwezo wa kulifanya taifa kuwa na sifa ya kuwavutia wawekezaji kuingia nchini bila kuwa na shaka yoyote, jambo ambalo litafanya nchi kuwa katika hali ya utulivu," alisema Misime.

Alisema waandishi wakishirikiana vyema na Jeshi la Polisi hasa katika kufichua au kutoa taarifa sahihi, ni wazi taifa na wananchi wake watakuwa salama.

Awali, Mkurugenzi wa UTPC, Kenneth Simbaya, alisema ni haki kwa mwandishi wa habari kufanya kazi yake katika mazingira rafiki bila bughudha toka kwa mtu yeyote.

Alisema kama mwandishi atakuwa anafanya kazi kwa kunyimwa uhuru, itasababisha Watanzania kukosa habari na mwandishi mwenyewe kushindwa kutimiza wajibu wake kikamilifu.

Vilevile, alisema mwandishi wa habari anatakiwa kufanya kazi kwa kupewa uhuru na kulindwa na kuwekewa mazingira rafiki kwa lengo la kutimiza majukumu yake ya kila siku kwa manufaa ya taifa.

"Ninaamini mdahalo huu utasaidia kutengeneza msingi mzuri kwa waandishi wa habari katika kutimiza majukumu yao ya kila siku kwa uhuru na kuzingatia maslahi mapana ya taifa," alisema Simbaya.

Rose Reuben, Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Waandishi Wanawake Tanzania (TAMWA), alisema asilimia 64 ya wanawake waliomo katika vyumba vya habari mkoani Dar es Saalam wamefanyiwa unyanyasaji wa kingono.

"Unyanyasaji huo, ikiwamo rushwa ya ngono na sababu kubwa, ni ili kazi zao ziweze kutoka katika vyombo vya habari na wengine ili wapate kazi za nje ya mkoa," alisema.

Aliongeza kuwa wanawake wengine wamejikuta wakiingia katika ukatili wa kingono katika vyumba vyao vya habari kutokana na hofu ya kupoteza kazi zao.

"Kukosa kujiamini kwa wanawake katika vyumba vya habari na kushindwa kuelezea madhila wanayokumbana nayo katika kazi zao, kumeendelea kuleta ugumu katika kupambana na matukio ya ukatili na rushwa ya ngono," alisema.

Rose alisema ni vyema kutoa taarifa ya matukio kama hayo ili kutoa nafasi ya kushughulikiwa.





# Utekelezaji makuzi mtoto waleta matokeo chanya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UTEKELEZAJI wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMAMA) umeanza kuleta matokeo chanya kutokana na ufuatiliaji wa karibu wa wajawazito kuhakikisha wanapata vipimo vya msingi.

Programu hiyo inaelezwa kuwa imeanza kuleta matokeo chanya kwa wajawazito wilayani Chunya kujifungua watoto wenye afya bora ambayo ni miongoni mwa matokeo yanayotakiwa.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa programu hiyo kwenye kikao cha tathmini ya robo ya tatu ya PJT-MMMAM mkoa wa Mbeya, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Chunya, Nasra Mkupete, alisema kwa sasa kuna mwitikio mkubwa wa wajawazito kupima afya zao.

Alisema wadau kwa kushirikiana na vituo vya kutolea huduma za afya wamekuwa wakishirikiana kuhakikisha wajawazito wanahudhuria kliniki na kupima afya zao kwa kuhakikisha jamii inapewa elimu, ukusanyaji wa taarifa za wajawazito wanaopata vipimo na ufuatiliaji wa mahudhurio kliniki.

**Matatizo ya makuzi ya watoto yamekuwa yakionekana pia kwenye familia za watekelezaji wa programu hiyo jambo ambalo linaweza likafikisha malengo ya serikali.**

Vipimo vya afya kwa wajawazito, alisema vinalenga kubaini uwapo wa magonjwa yanayoweza kusababisha mtoto kukosa afya bora anapozaliwa na kwamba vipimo vinavyozingatiwa zaidi ni vya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), kaswende, wingi wa damu na malaria.

"Shughuli nyingine iliyofanyika ni kufuatilia watoto wote waliozaliwa katika kipindi cha kati ya Aprili na Juni kuona kama walipata chanjo. Hii tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa sababu mpaka sasa watoto wenye umri chini ya miaka mitano wote wamepata chanjo," alisema Mkupete.

Alisema malengo ya mpango huo kwa robo ya tatu yalikuwa kuwafikia wajawazito 5,581 katika kipindi cha Apriri hadi Juni, mwaka huu na kwamba yamefikiwa kama ilivyopangwa.

Ofisa huyo alisema shughuli nyingine iliyofanyika katika kipindi hicho ni kufanya mafunzo rejea juu ya dalili za hatari katika vituo vyote 37 vinavyotoa huduma ya Mama na Mtoto wilayani humo.

Awali, akifungua kikao hicho, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Joel Mwakapala, alisema serikali inataka matokeo chanya ya programu hiyo yaanze kuonekana kuanzia kwenye familia za watendaji wanaoitekeleza.

Mwakapala alisema matatizo ya makuzi ya watoto yamekuwa yakionekana pia kwenye familia za watekelezaji wa programu hiyo jambo ambalo linaweza likafikisha malengo ya serikali.

Ofisa Mawasiliano na Ushirikiano wa Mtandao wa Maendeleo ya Awali ya Mtoto Tanzania (TECDEN), Andrew Nkunga, alisisitiza umuhimu wa wadau yakiwamo mashirika binafsi kushirikishwa kwenye utekelezaji wa programu hiyo kwa kuwa mchango wao unahitajika.

Kwa mkoani Mbeya, PJT-MMMAM ilizinduliwa Agosti 19, mwaka jana, ikiwa sehemu ya mikoa 10 ya awali iliyoanza utekelezaji wa programu hiyo nchini na tayari matokeo katika baadhi ya maeneo yameanza kuonekana kwenye vipengele vitano vya malezi jumuishi.



Mbunge wa Viti Maalumu anayetokana na vyama vya wafanyakazi, Dk. Alice Kaijage (kulia), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Renatus Mchau, kabla ya kukutana na baadhi ya wafanyakazi wa wilaya hiyo alipokuwa katika ziara mkoani humo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## RC ahadharisha uuzaji wa mbolea feki

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI mkoani Njombe imetahadharisha kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara watakaobainika kuwauzia wakulima mbolea feki huku ikisisitiza kuwa vitendo hivyo ni kuhujumu jitihada za serikali za kuwainua wakulima.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waumini wa Kanisa la Waadvetista Wasabato ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya Sikukuu ya Makambi yanayofanyika viwanja vya Sabasaba mjini hapa.

"Mwashauri wafanyabiashara wa mbolea ninyi wazawa wa Njombe wasiingie kuwauzia mbolea feki. Serikali ina mkono mrefu, jicho la serikali liko kila mahala. Tusije tukalaumiana kwa mtu aliyeuza mbolea feki, hatutakua na msamaha wa aina yoyote," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka wananchi mkoani hapa kutafuta njia bora ya kutatua migogoro na si kuuana kwa sababu visasi kwenye familia na biashara ni sababu kubwa zinazochangia kuwapo kwa matukio hayo.

"Niwaombe tujiepushe na kulipizana visasi. Kama mashamba ya miti umeambiwa kwamba baba yako alipofariki (dunia) mama yako aliachiwa miti akadhulumiwa na mashemeji zake, tafuta namna nzuri ya kupata haki ya miti ya baba yako. Usiende kuichoma wala usiende kukodi watu kwa ajili ya kwenda kumuua baba mdogo wala mjomba," alisema Mtaka.

Mtaka pia aliwataka wanafunzi wanaojiandaa na mitihani ya kidato cha pili na cha nne kwamba ili wafaulu wanapaswa kusoma kwa bidiii na si vinginevyo.

Awali, Katibu Mkuu NGDF ambaye ni Mnenaji Mkuu wa Makambi, Mchungaji Richard Mashauri kutoka Kahama mkoani Shinyanga, alisema waumini wanapaswa kupinga mauaji ya vikongwe, watoto, ushonga na utajiri kwa njia ya miujiza.

# TFRA yaelimisha matumizi ya mbolea Songwe

**Na Renatha Msungu,** MOMBA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa kushirikiana na wataalamu wa Wizara ya Kilimo na vyama vya ushirika, imeweka kambi ya siku 14 katika wilaya ya Momba mkoani Songwe kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea.

Elimu hiyo inatolewa kuondoa dhana potofu iliyoko miongoni mwa wananchi wa maeneo hayo kwamba matumizi ya mbolea za kisasa yanaharibu udongo.

TFRA imeanza kutoa elimu hiyo kabla msimu mpya wa kilimo haujaanza ili wakulima waanze utekelezaji msimu ujao na wafanye kilimo chenye tija ambacho kitawainua kiuchumi na kuwa na uhakika wa chakula.

Mtaalamu wa masuala ya mbolea kutoka TFRA, Henerico Renatus, alisema wakulima wanapaswa kuachana na mawazo kuwa mbolea inaharibu udongo na badala kuchangia kuongeza uzalishaji wa mazao.

"Mawazo hayo yamekuwa yakiwachelewesha wakulima kufikia mafanikio. Kwa karne hii huwezi kukwepa matumizi ya mbolea. Kwanza ardhi imechoka inahitaji kuongezewa rutuba kupitia mbolea," alisema Renatus.

Naye Daniel Maarifa, mtaalamu wa mbolea, alisema wakulima wanapaswa kuondokana na kilimo cha mazoea badala yake waendeshe kilimo cha kisasa ambacho wakulima hutumia mbolea ikiwamo kufuata kanuni za kilimo kutoka kwa wataalamu wa sekta hiyo.

Maarifa alisema kilimo cha kisasa cha kufuata kanuni kinachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza tija katika uzalishaji lakini kinaleta matokeo chanya kwa wakulima.

Mratibu wa Utafiti na Ubunifu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Ilonga, Meshack Makenge, alisema mafanikio mengine katika kilimo ni wakulima kuzingatia uchaguzi sahihi wa mbegu na kupanda kwa utaalamu zaidi.

Mratibu wa Uhawilishaji wa Teknolojia na Uhusiano wa TARI-Ilonga, Lilian Mwanga, alisema katika kuwasaidia wa kulima, taasisi hiyo inazo teknolojia mbalimbali za kisasa zinazomwezesha mkulima kufikia mafanikio ya haraka kupitia sekta ya kilimo.

"Tunapozungumzia teknolojia ni pamoja na mbegu bora za mazao mbalimbali, zikiwamo mahindi, alizeti, mtama, ufuta na mazao yote ya mikunde ambayo kwa asilimia kubwa taasisi yetu inazalisha," alisema Mwanga.

Mbunge wa Momba, Condester Sichalwe, alisema wakulima wanapaswa kuwa na mwamko wa kutumia mbolea ili kupiga hatua katika kilimo.



# Wenye ulemavu waomba pensheni maalum

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATU wenye ulemavu Mkoa wa Kaskazini Unguja wameiomba serikali kuwawekea pensheni maalum ili kujikwamua na hali ngumu ya maisha.

Walisema hayo wakati wakizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, katika mikutano yake ya kusikiliza kero za wananchi wa mkoa huo, uliofanyika katika viwanja vya soko la wajasiriamali, Kinduni mkoani humo.

Pia walisema serikali imetenga fedha maalum kwa wazee, pensheni jamii ambayo hupewa kila mwisho wa mwezi na kwamba ni vyema watu wenye ulemavu wakapatiwa fursa hiyo.

**Watu wengi wenye ulemavu wanakabiliwa na ukosefu wa kipato kutokana na kutokuwa na biashara au ajira za kuwasaidia na familia zao.**

"Serikali inatoa Sh. 50,000 kwa kila mzee aliyefikisha umri wa miaka 50 kila mwisho wa mwezi kwa ajili ya kujikimu kimaisha, tunaomba na sisi watu wenye ulemavu kupatiwa fedha ya kujikimu kwa sababu maisha yetu ni magumu," alisema Abdulfatah Kudura Makame.

Aidha, alisema kama utakuwapo utaratibu wa kuwawezesha watu wenye ulemavu kwa kuwapatia kiwango cha fedha ya kujikimu kila mwisho wa mwezi, tatizo la ombaomba litakuwa ni historia.

Alisema baadhi ya watu wenye ulemavu hulazimika kuwa ombaomba mitaani kwa sababu ya ugumu wa maisha huku familia ikimtegemea kwa mahitaji mbalimbali.

Alisema watu wengi wenye ulemavu wanakabiliwa na ukosefu wa kipato kutokana na kutokuwa na biashara au ajira za kuwasaidia na familia zao.

"Mkuu wa mkoa usituone tuna mvi kichwani udhani ni uzee, hapana hii ni njaa wananchi wako tuna maisha magumu njaa kali na ajira hatuna," alisema.

Hata hivyo, alisema mfumko wa bei za bidhaa ni changamoto kubwa kwa wananchi wa mkoa huo na gharama za maisha zimepanda.

Mkuu wa Mkoa, Ayoub Mohammed Mahamoud, alisema uongozi wa mkoa utafanya juhudi za kuwawezesha watu wenye ulemavu ikiwamo kuwapatia mikopo na mitaji ili kufanya biashara na kuachana na utegemezi.

Akizungumzia mfumko wa bei, Ayoub alisema hali hiyo kwa bidhaa za vyakula inatokana na kupanda kwa dola, pia kuongezeka kwa mfumuko wa bidhaa duniani kunatokana na sababu mbalimbali.

Katika mkutano huo pia ziliibuka baadhi ya changamoto ikiwamo kutokuwapo kwa miundombinu ya kupitisha maji ikiwamo mitaro katika barabara kuu kutoka Nungewi hadi Mahonda hali ambayo imesababisha wakati wa mvua maji kuvamia makazi ya wananchi.

## Siku ya Amani Duniani kufanyika Zanzibar leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAADHIMISHO ya Siku ya Amani Duniani yanatarajiwa kufanyika leo visiwani hapa na katika kongamano hilo mada mbalimbali zitajadiliwa ikiwamo uwezeshwaji wa vijana katika kuleta amani na namna ya kujenga jamii yenye amani.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho hayo, Ofisa Habari kitaifa kutoka kituo cha habari cha Umoja wa Mataifa (UN) Nafisa Ddidi, alisema maadhimisho hayo yataambatana na kongamano ambalo litawashirikisha watu mbalimbali ikiwamo vijana.

Alisema maadhimisho hayo pia yanakwenda sambamba na shughuli mbalimbali ikiwamo utoaji wa elimu kwa vijana na wanafunzi shuleni pamoja na upandaji wa miti aina ya mikoko katika fukwe za bahari visiwani hapa.

Naye Canon Christopher, Mwenyekiti wa umoja wa makanisa Zanzibar, alisema amani ni kinga na ngao, inapokesekana huwa na vita na machafuko.

Alisema hata vitabu vya dini vimehimiza suala la amani kwa sababu ikitamalaki kutakuwa na upendo na kuishi kwa utulivu.

Idi Hussein Idi, kutoka Ofisi ya Mufti Zanzibar alisema viumbe na binadamu wanahitaji kuishi kwa amani na hata vitabu vya dini vimeeleza umuhimu wa amani.

Alisema inapokuwapo amani nchini maendeleo, uchumi na uwekezaji huimarika kwa sababu wageni huwekeza nchini na kupata maendeleo.

"Amani inapoimarika katika nchi, maendeleo huwapo kila kona na wananchi huishi bila ya hofu."

Aidha, alisema viongozi wa nchi wanahimiza amani kwa sababu Tanzania ina amani na wageni kutoka mataifa mbalimbali hufika kujifunza mambo mbalimbali.

Kelvin Adward, Katibu wa asasi ya vijana Tanzania, alisema vijana wana nafasi kubwa ya kutoa elimu na kuwataka kutokubali kutumika kuvunja amani iliyopo kwa sababu hakuna mbadala wake.

Alisema vijana lazima wewe mfano wa kuigwa katika jamii katika kuimarisha amani iliyopo na maadhimisho hayo itatoa fursa nzuri kwa vijana.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation, Asma Ali Hassan Mwinyi (wa pili kulia) na Meneja Masoko wa Benki ya Exim Tanzania, Kauthar D'souza (wa pili kushoto), wakisaidia kumtwisha ndoo ya maji kichwani mkazi wa Tumbatu, wakati wa uzinduzi wa mradi wa majisafi na salama unaofadhiliwa na benki hiyo, utakaonufaisha zaidi ya kaya 5,000 katika Kijiji cha Tumbatu Unguja, Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali sasa kutoa ufadhili wa masomo nje ya nchi kwa fani adimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema imesitisha usajili wa ufadhili kwa masomo katika vyuo vya elimu ya juu nje ya nchi isipokuwa kwa fani adimu ambazo hazipatikani nchini.

Hayo yalisemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa wizara hiyo, Lela Muhamed Mussa, wakati akiwasilisha ripoti ya wizara hiyo kupitia kamati ya ustawi wa jamii kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema, uamuzi huo umefikiwa na serikali na Bodi ya Mikopo imetakiwa kusitisha usajili wa masomo katika vyuo vya nje isipokuwa kwa taaluma chache ambazo hazipatikani katika vyuo vya ndani.

Alisema, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Muungano katika elimu ya juu pamoja na Bodi ya Mikopo ya Jamhuri ya Muungano, wamekubaliana kuwapatia nafasi za masomo wanafunzi wa Zanzibar katika masomo ya aina mbalimbali.

Alisema wanafunzi kutoka Zanzibar wamejiunga na kupata elimu ya juu katika vyuo vya elimu ya juu kutoka Tanzania Bara ikiwamo Chuo kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Benjamin Mkapa, Dodoma pamoja na taasisi za elimu ya juu katika masuala ya bahari ya sayansi na ardhi.

Mussa alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia ufadhili wa Benki ya BADEA inatarajia kujenga majengo mengine manne katika kampasi ya Chuo Kikuu cha Tunguu, mradi ambao unatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kinatarajia kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa ukarabati wa miundombinu.

Pia alisema chuo kimetenga jumla ya Shilingi bilioni nne kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la shule ya kinywa na meno katika kampasi ya Tunguu ya Chuo cha Afya Sayansi na tiba kwa ajili ya kufundisha wanafunzi wake.

Alisema, Chuo cha Sayansi na Tiba kinahitaji jumla ya wataalamu 74 kwa ajili ya kuendesha masomo yanayohusiana na kada hiyo.

Alisema kwa sasa wanaendelea kuwatumia wataalamu na walimu kutoka nje ya nchi wapatao 13 ikiwamo kutoka Cuba, Nigeria pamoja na China.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**SAID NASSORO UWEMBA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE339925** iliyotolewa mwaka 12/05/2020 na makao makuu DAR ES SALAAM PCO. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHA/RB/710299/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA TELLA LA GARI

**NGABANYA GILU MIGANGALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya **TELLA** la gari lenye namba za usajili **T. 855 CKU.** Yeyote atakayeiona ataoe taarifa kituo cha polisi kilicho jirani yake. Taarifa ya polisi. **KAH/TR/RB/662/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA TELLA LA GARI

**ALPHAXARD KANGI LUGOLA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISH FUSO** yenye jina la umiliki **MWIBARA INVESTMENTS LIMITED** yenye usajili namba **T 454 BRS.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/MAR/BUN/466/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUMA ALLY SHUMBU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 970 DGU.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/257687/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**ALUTA MUSSA NYAGANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya mbili za gari ya kwanza yenye majina **CHARLES MARCO MAMUYA** namba za usajili **T234DFB** aina ya **MAZDA BRAWNY** Chassis No. **S,D89T501572,** na ya pili yenye majina **LUGE GEORGE NYONGO** Namba za usajili **T594DGK** aina ya **SUZUKI CARRY,** Chassis No. **DD511536957.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/3316/2023**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ALEX GERALD HERUKA** anatangaza kupotelewa kwa Hati ya Kusafiria yenye Namba **TAE259956** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es Salaam tarehe 12/12/2019 ambayo itaisha tarehe 11/12/2029. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/12973/2023.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KIJAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TANGA**

**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 166/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU DANIEL GASPER DANIEL**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARIA DANIEL GASPER**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 Mwezi wa 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 20 Mwezi wa 09 Mwaka 2023.**

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI TANGA

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI ...... ...70...... LA.... 2023**

**HARMAS LAIT KIWIA ...............MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JOANNA FRANSYCER CHIFUNDA...MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**JOANNA FRANSYCER CHIFUNDA**
**POPOTE ULIPO/MLIPO:**

**HARMAS LAIT KIWIA** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 18/10/2023 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 19 Mwezi .....09....,2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na..../2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU RASHID MOHAMED wa CHINANGARI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA MUHAMMAD RASHID UPANGA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo Tarehe 18 Mwezi 09 Mwaka 2023.**

---

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.119 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late PHILIPO MINAELI MFINANGA of Chinyoyo-Kilimani within Dodoma city**

**And**

**In the matter of application for letters of Administration by JANETH JUSTINE MGHAMBA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 19 Day of October, 2023

Dated at Dodoma this 19 day of September, 2023

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/C
DODOMA DISTRICT

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TANGA**

**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 165/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SALIMU SHAMIS SALUMU**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SLIMA SALIMU SHAMIS**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **26 Mwezi wa 09 Mwaka 2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 19 Mwezi wa 09 Mwaka 2023.**

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MKINGA**

**Kituo cha MKINGA P/CRT Mkoa ..............**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 03/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAMISI JOGA JENKE wa GERE - GOMBERO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HUSSEIN HAMISI JOKA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **27 Mwezi wa 09 Mwaka 2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 19 Mwezi wa 09 Mwaka 2023.**

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Kagame: Nitagombea urais muhula wa nne

**Kigali, RWANDA**

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame, amesema atawania muhula wa nne katika uchaguzi wa rais mwakani.

"Ndiyo, hakika mimi ni mgombea." Kagame aliliambia jarida la lugha ya Kifaransa la Jeune Afrique.

Alipoulizwa kuhusu nchi za Magharibi zitachukulia vipi uamuzi wake wa kugombea tena, Kagame alisema, "Samahani kwa nchi za Magharibi, lakini kile ambacho nchi za Magharibi hufikiri si tatizo langu."

"Nimefurahishwa na imani ya Wanyarwanda kwangu. Nitawatumikia daima, kadri niwezavyo."

Aprili mwaka huu, Rais Kagame alinukuliwa akisema kwamba anatazamia kustaafu na kukabidhi madaraka baada ya miaka 23 madarakani.

Chama tawala nchini humo, Rwandan Patriotic Front (RPF-Inkotanyi), kilimuacha Kagame kuendelea kuhudumu kama mwenyekiti wake. Ameongoza chama hicho tangu mwaka 1998.

Kagame amekuwa rais wa taifa hilo la Afrika Mashariki, tangu mwaka 2000. Kura ya maoni iliyozua utata mwaka 2015, iliondoa ukomo wa mihula miwili ya kikatiba kwa marais.

Alishinda uchaguzi uliopita wa 2017 kwa asilimia 98.8 ya kura.

Rwanda chini ya Rais Kagame, imekuwa na utulivu wa kisiasa, ingawa wakosoaji na makundi ya haki za binadamu yanaituhumu serikali yake kwa kuweka mipaka ya uhuru wa kisiasa na kukandamiza upinzani. **BBC**



Rais Paul Kagame. **PICHA: MTANDAO**

# EU yaondoa misaada kwa ufujaji

**Nairobi, KENYA**

UMOJA wa Ulaya (EU), umethibitisha kusitisha kwa muda malipo kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), kwa ajili ya kutoa misaada ya kibinadamu nchini Somalia.

Msemaji wa Tume ya Umoja wa Ulaya, Balazs Ujvari, amesema hatua hiyo imechukuliwa kama njia mojawapo ya kulinda fedha za EU.

Uchunguzi uliofanywa na Umoja wa Mataifa (UN), ulibaini kuwapo kwa wizi wa misaada inayotolewa, maofisa usalama pia wafanyakazi wa misaada wanahusishwa na sakata hilo.

Mwaka jana, EU ilitumia zaidi ya dola milioni saba, sawa na paundi milioni 5.6 kwa ajili ya kuendeleza shughuli za WFP nchini Somalia.

Kwa upande wake Shirika la Misaada la Marekani (USAID), limesema halina mpango wa kusitisha msaada wa utoaji wa chakula kwa Somalia.

Mamilioni ya watu nchini Somalia, wanahitaji chakula cha msaada kutokana na ukame wa muda mrefu katika pembe ya Afrika, pamoja na usalama duni, unaosababishwa na wapiganaji wa Al Shabab, huku idadi kubwa ya raia wakienda kuishi katika kambi za wakimbizi.

**RFI**

# Muswada wapendekeza LGBTQ jela miaka 50

**Nairobi, KENYA**

MUSWADA unaopendekezwa dhidi ya wapenzi wa jinsia moja, unataka watu wa mapenzi ya jinsia moja, kufungwa jela miaka 50 kwa kufanya mapenzi bila ridhaa.

Unaitwa, Muswada wa Ulinzi wa Familia wa 2023. Rasimu ya sheria inayofadhiliwa na mbunge wa Homa Bay Town, Peter Kaluma, inapendekeza kupiga marufuku mapenzi ya jinsia moja, muungano wa watu wa jinsia moja na shughuli na kampeni zozote za LGBTQ.

Pia inalenga kupiga marufuku maandamano ya watu wa mapenzi ya jinsia moja, mikusanyiko na maandamano barabarani kadhalika mavazi yanayoashiria mhusika wa jinsia moja hadharani.

"Mtu anayeshiriki tendo la ndoa na mtu wa jinsia moja, bila ridhaa ya mtu mwingine akipatikana na hatia atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka 10 na kisichozidi miaka 50," umesema muswada huo.

Wamiliki wa majengo yanayotumika kwa mapenzi ya jinsia moja, watalipa faini ya dola za kimarekani 14,000 au watakabiliwa na kifungo cha miaka saba jela, iwapo muswada huo utakamilika.

Wiki iliyopita, makasisi na baadhi ya mashirika ya kijamii yalifanya maandamano ya kupinga LGBTQ katika mji wa Mombasa.

Hii ilikuja kutekelezwa tena na Mahakama ya Juu ya Kenya, kwa uamuzi wa katikati ya Septemba mwaka huu, kuruhusu usajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali ya LGBTQ.

Bodi ya Kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Kenya, ilikataa kusajili Tume ya Kitaifa ya Haki za Watu wa Mapenzi ya Jinsi moja, ikisema inakuza tabia ya watu wa jinsia moja.

Mahakama ya Juu, mapema mwaka huu, ilichukulia hatua hiyo kuwa ya kibaguzi na kinyume na katiba, hivyo basi kuruhusu mashirika ya LGBTQ kujiandikisha katika uamuzi wa kihistoria.

**BBC**

# Mtoto wa Rais Ali Bongo ashtakiwa kwa uhaini

**Libreville, GABON**

MWENDESHA Mashtaka wa Serikali Gabon, anasema mtoto wa kiume mkubwa wa rais aliyeondolewa madarakani, Ali Bongo na washirika wake kadhaa wa kisiasa, wamefunguliwa mashtaka ya uhaini na rushwa.

Noureddin Bongo Valentin, mwenye umri wa miaka 31, alikamatwa muda mfupi baada ya mapinduzi ya mwezi uliopita.

Televisheni ya Taifa ilionesha picha zake na baadhi ya washirika wa karibu wa baba yake, wakiwa mbele ya masanduku ya pesa ikidaiwa yalikuwa yamenaswa kutoka katika nyumba zao.

Wenyewe hawajazungumzia lolote kuhusu tuhuma hizo. Jeshi lilichukua mamlaka baada ya Ali Bongo kutangazwa mshindi wa uchaguzi wa urais wa Gabon.

Bongo, amekuwa ofisini tangu mwaka 2009 alipomrithi baba yake ambaye alitawala nchi hiyo kwa miaka 41.

Gabon, imeondolewa kwa muda katika Jumuiya ya Madola, baada ya makamanda wa kijeshi kufanya mapinduzi yaliyomwondoa madarakani Rais Ali Bongo.

Uamuzi huo umetolewa na mawaziri wa mambo ya nje wa Jumuiya ya Madola, waliokutana baada ya mkutano mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN).

**BBC**

# CHAMA AINGIA KUMI BORA LIGI YA MABINGWA AFRIKA

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO wa Simba, Clatous Chama, ameingia kwenye orodha ya 10 bora ya wafungaji bora wa wakati wote wa Ligi ya Mabingwa Afrika akiwa amefikisha mabao 17.

Kwa mujibu wa mtandao ya 'Transfermartket' Chama anashika nafasi ya tisa kwenye orodha ya wafungaji bora wa muda wote kwenye ligi hiyo.

Chama ameingia kwenye orodha hiyo kufuatia mabao mawili aliyoifungia Simba kwenye mchezo wa kwanza wa ligi hiyo kuwania kutinga hatua ya makundi dhidi ya Power Dynamos uliochezwa Jumamosi iliyopita Ndola, Zambia.

Katika orodha ya wachezaji hao wenye mabao mengi, nahodha waTimu ya Taifa 'Taifa Stars', Mbwana Samatta akishika nafasi ya tano akiwa na mabao 20.

Mshambuliaji wa zamani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na klabu ya TP Mazembe, Tresor Mputu, anaongoza orodha hiyo akiwa na mabao 31 sawa na mshambuliaji wa zamani wa Al Ahly na Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Aboutreika.

Nafasi ya tatu kwenye orodha hiyo ya wachezaji 10 wenye mabao mengi inashikwa na Emas Meteb mwenye mabao 24, Muangola Flavio anashika nafasi ya nne akiwa na mabao 21 huku Dioko Kaluyituka akishika nafasi ya sita na mabao 19 akifuatiwa na Edward Sodombo mwenye mabao 18.

Mshambuliaji wa zamani wa Al Ahly, Walid Soliman anashika nafasi ya nane akiwa na mabao 17 sawa na Chama anayeshika nafasi ya tisa.

Winga wa zamani waAl Ahly, Mohamed Barakat, anafunga orodha ya 10 bora akiwa na mabao 16.

## KMC yaifungia kazi Geita Gold FC

**Na Saada Akida**

BAADA ya ushindi kwenye mchezo uliopita dhidi ya JKT Tanzania, Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moalini, amesema kikosi chake kipo imara na wapo tayari kusaka pointi tatu kwenye mchezo wao unaofuata dhidi ya Geita Gold FC.

Moalin alisema tayari wachezaji wake wameingia kambini kujiandaa na mchezo huo utakaochezwa Septemba 30.

Akizungumza na Nipashe jana, alisema maandalizi yao yanaendelea vizuri wachezaji wote wamerejea kambini kujiandaa kwa ajili ya kusaka pointi tatu ugenini mbele ya Geita Gold.

Alisema anashukuru mpaka sasa hana rekodi ya majeruhi na kazi aliyonayo ni kufanyia kazi mapungufu aliyoyaona kwenye mechi zilizopita.

"Hadi sasa hatuna majeraha tumeendelea na maandalizi yetu kufanyia kazi changa moto zilizojitokeza kwenye mechi ya awali, niliona kasoro kidogo kwenye safu yetu ya kiungo na ulinzi, tunaendelea kufanyia kazi, tunahitaji matokeo mazuri ugenini," alisema kocha huyo.

Alisema wanatarajia kuondoka Dar es Salaam, Septemba 23 kuelekea Mwanza ambapo wataweka kambi ya siku chache kabla ya kuelekea Geita siku moja kabla ya mchezo.

KMC inashika nafasi ya nane ikiwa pointi nne ikicheza mechi tatu, imeshinda mmoja, sare moja na imepoteza mchezo mmoja.






Wachezaji wa Azam FC, Prince Dube (kushoto) na Abdul Sopu, wakifanya mazoezi ili kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Fountain Gate itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Ngumi ufukweni sasa kufanyika Oktoba Msasani

**Na Shufaa Lyimo**

MAPAMBANO ya ngumi za ufukweni yaliyokuwa yafanyike Oktoba 28 kwenye fukwe za Msasani jijini Dar es Salaam 'Safari ya Beach' yamerudishwa nyuma na sasa yatafanyika Oktoba 22 mwaka huu.

Mbali na kurudisha nyuma kwa siku tano, pia yamebadilishiwa eneo na sasa yatafanyika Rongoni, Kigamboni.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, mratibu wa mapambano hayo, Meja Selemani Semunyu alisema wameamua kuyapeleka mapambano hayo kwenye fukwe za Rongoni Kigamboni kutokana na maombi ya wadau wengi.

"Tumepokea maombi mengi ya wadau kuhusu eneo linalostahili ngumi hizi kufanyika, kama waandaaji tumeamua kuyafanyia kazi maombi yao na sasa yatafanyika Rongoni na tunaamini kila kitu kitakwenda sawa," alisema Meja Semunyu.

Aidha, alisema maandalizi yanaendelea vizuri kuelekea kwenye mapambano hayo ambayo yanatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa.

Alisema vijana wataonyesha vipaji ambavyo kila mdau wa mchezo wa ngumi atapata burudani.

"Naomba wadau wa ngumi waje kwa wingi siku hiyo, kutakuwa na burudani nyingi zitakazotolewa na vijana wetu," alisema .

## Mafunzo yajifariji Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa Mafunzo SC, Abdallah Bakari 'Edo', amesema licha ya kupoteza pointi kwenye michezo miwili ya kwanza ya Ligi Kuu ya Zanzibar, bado hawajajiondoa kwenye mbio za ubingwa msimu huu.

Edo alisema lengo lao msimu huu ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na bado lengo hilo wanalo.

Mafunzo, juzi ilipokea kipigo cha kwanza baada ya kufungwa bao 1-0 na Kundemba katika mchezo wa mzunguko wa pili wa ligi hiyo ya PBZ ukifuatiwa mchezo wao wa kwanza ambao walitoka sare.

Akizungumza na gazeti hili, Edo, alisema kwa kawaida michezo ya mwanzo ya ligi inakuwa migumu na timu zote zinakuwa na hamasa kubwa ya kusaka matokeo.

Alisema katika mchezo wao dhidi ya Kundemba timu yao ilicheza vizuri katika dakika zote hata bao lililofungwa lilikuwa la dakika ya mwanzo licha ya kushindwa kupata matokeo.

"Tulicheza vizuri sana, na wachezaji walijituma bila ya kuchoka ila kikubwa niseme bahati haikuwa kwetu, tunajipanga kwa mchezo ujao kuziba mapungufu ya michezo miwili tuliyocheza," alisema Edo.

## ZISIKUPITE

### KANE KUREJEA SPURS

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy amefichua klabu hiyo ina kipengele cha kumnunua tena mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 30, iwapo ataondoka Bayern Munich. **(Fooball.London)**

### MADRID ILIMTAKA KANE

REAL Madrid walikuwa wameweka dau la pauni milioni 60 kumnunua, Harry Kane kabla ya nahodha huyo wa England kuhamia Bayern Munich msimu huu huku Paris St-Germain nao wakituma ombi. **(The Athletic)**

### TONEY AWEKWA SOKONI

KOCHA wa Brentford, Thomas Frank amesema atafikiria kumuuza mshambuliaji wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27 Januari kama bei itakuwa sawa. **(Sky Sports)**

### TONEY AGEUKA LULU

KLABU za Arsenal, Chelsea na Tottenham Hotspur zinavutiwa na Ivan Toney huku Brentford ikiwa tayari kumruhusu mchezaji huyo kuondoka kwa ada ya pauni milioni 60. **(Mirror)**

### VICKERS ANUKIA ARSENAL

ARSENAL ilituma wasaka vipaji wake katika mechi ya Reading ya EFL dhidi ya Exeter iliyochezwa juzi huku washikabunduki hao wakiwa na nia ya kumnunua mshambuliaji wa England, Caylan Vickers mwenye umri wa miaka 18 na mlinzi wa New Zealand, Tyler Bindon (18). **(Express)**

### BYNOE-GITTENS KUTUA ARSENAL

ARSENAL pia inavutiwa na mshambuliaji wa England, Jamie Bynoe-Gittens mwenye umri wa miaka 19 anayeichezea klabu ya Borussia Dortmund. **(Fichajes kupitia Daily Star)**

### BARCO KUBAKIA BOCA

KLABU ya Boca Juniors ina matumaini ya kumpa mkataba mpya mlinzi wa Timu ya Taifa ya Argentina, Valentin Barco mwenye umri wa miaka 19, licha ya Brighton kuonyesha nia ya kumhitaji. **(90min)**

### KONSA, VILLA KIMEELEWEKA

ASTON Villa ipo katika mazungumzo ya kumpa mkataba mpya beki wa Timu ya Taifa ya England, Ezri Konsa mwenye umri wa miaka 25. **(Mail)**

### VERMEEREN KUTUA BARCA

BARCELONA imeonyesha nia ya kumnunua kiungo wa Royal Antwerp, Arthur Vermeeren huku Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 18 akitajwa kuwa Sergio Busquets ajaye. **(90min)**

### IBRAHIMOHIC KUULA MILAN

MMILIKI wa Klabu ya AC Milan, Gerry Cardinale, alikutana na kuzungumza na mshambuliaji wa zamani wa timu hiyo, Zlatan Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 41, kuhusu nafasi ya uongozi kwenye bodi. **(Football Italia)**

### TERRY KUREJEA CHELSEA

NAHODHA wa zamani wa Chelsea, John Terry mwenye umri wa miaka 42, yuko katika kundi linalotaka kununua asilimia 10 ya hisa katika klabu hiyo huku mmiliki mwenza, Todd Boehly akiwa tayari kwa uwekezaji mpya. **(Telegraph)**

### ANTONIO KUBAKIA WEST HAM

MSHAMBULIAJI wa West Ham, Michail Antonio mwenye umri wa miaka 33 ana nia ya kusalia hapo kwenye Uwanja wa London na anataka kusaini mkataba mpya na klabu hiyo. **(Football Insider)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AFURAHIA UBORA WA ALVAREZ

Asema City imelamba dume katika usajili wa mshambuliaji huyo...

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola alimsifia, Julian Alvarez baada ya bao la pili la mshambuliaji huyo kuhamasisha ushindi wa magoli 3-1 ambao Manchester City imeupata katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Crvena Zvezda iliyochezwa juzi usiku.

City walitanguliwa na wageni wao kutoka Serbia hadi muda wa mapumziko, lakini Alvarez alisawazisha dakika mbili za kipindi cha pili na dakika chache baadaye kuongeza la pili.

Na Guardiola alifichua jinsi alivyokuwa na shukrani kwa mabosi wake kwa kumleta mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 klabuni hapo.

Bosi huyo wa City alisema: "Ni usajili bora ambao klabu imefanya.

"Yeye ni mdogo sana na ana kila kitu. Kupigana, kufunga mabao, kutoa pasi za mabao na ni mtu wa ajabu na mzuri.

"Akicheza nyuma ya Erling ni tishio la ajabu. Bao lake la kwanza lilikuwa zuri sana, mwendo wake ulikuwa wa haraka sana.

"Msimu uliopita tulikuwa na Kevin (De Bruyne) na Ilkay Gundogan katika nafasi hiyo na walikuwa wa ajabu. Wakati mwingine ilikuwa vigumu kupata nafasi lakini sikuwahi kuwa na shaka."

Guardiola pia alifurahishwa na nyota Rodri, akidai yeye ndiye kiungo bora zaidi duniani.

Mhispania huyo alifunga bao la tatu kwa City na kukamilisha ushindi wa mabao 3-1 na kocha wake hakusita kumsifu.

Alisema: "Kwa sasa, Rodri ndiye bora zaidi. Ni kiungo mkabaji wa kipekee.

"Tulikuwa na bahati tena klabu ikasajili mchezaji wa aina hii, alipofika hakuwa mchezaji wa aina hii, lakini sasa amecheza michezo mingi na ni mmoja wa manahodha wa timu."

Guardiola pia alifichua Bernardo Silva huenda akakosa mechi chache zijazo za City baada ya kutolewa nje kabla ya muda wa mapumziko.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno anaungana na John Stones, Mateo Kovacic, Kevin De Bruyne na Jack Grealish ambao ni majeruhi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,154,8

MECHI KALI
SIMBA S.C.
VERSUS
COASTAL UNION
1 | 1.18
X | 5.89
2 | 10.40

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Ally Saidi - 0655 067 XXX
2. Godifrey Lihokolelo - 0673 603 XXX
3. Zacharia Mollel - 0676 529 XXX
4. Ramadhani Juma - 0679 038 XXX
5. Haji Juma Hamisi - 0710 553 XXX
6. John Saga - 0712 345 XXX
7. Bedaso Mathayo - 0713 411 XXX
8. Onolina Tengelakwi - 0713 997 XXX
9. Alex Alex - 0717 153 XXX
10. Anna Balagwila - 0718 204 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI: BARCELONA SASA IMERUDI KATIKA UBORA

**BARCELONA, Hispania**



XAVI Hernandez amesema Barcelona kwa sasa wanacheza soka lao bora zaidi tangu achukue mikoba ya kuwa kocha baada ya kuwalaza Antwerp mabao 5-0 katika mechi ya ufunguzi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi.

João Félix alifunga mara mbili, huku Robert Lewandowski, Gavi na bao la kujifunga la Jelle Bataille likikamilisha karamu ya mabao na ikawa mara ya pili kwa Barca kufunga magoli matano ndani ya siku nne baada ya kuandikisha idadi kama hiyo dhidi ya Real Betis Jumamosi iliyopita.

"Nimefurahishwa sana na matokeo, lakini zaidi ya yote kwa jinsi tulivyocheza," alisema Xavi, ambaye alichukua nafasi ya Ronald Koeman kama kocha wa Barca Novemba, 2021 na kuiongoza klabu hiyo kutwaa ubingwa wa LaLiga msimu uliopita.

"Hatua za mapema usiku wa leo (juzi) ni kwa sababu hatukucheza vyema, lakini kuanzia dakika ya 20 nilifikiri tulidhibiti mchezo. Tulitawala kumiliki mpira, tuliokoa mipira ya juu na kushambulia vyema.

"Ni wazi kiwango cha timu hupanda wakati Ilkay Gündogan anacheza, João Cancelo anajua tunachotaka na Félix ameanza vizuri. Nadhani michezo hii miwili iliyopita ni kiwango bora zaidi ambacho tumeonyesha."

Kuwasili kwa Félix na Cancelo kumekuwa chachu ya ushindi wa Barca, huku wachezaji wote wapya waliosajiliwa wakivutia katika ushindi dhidi ya Betis na Antwerp.

"Ana mikoba ya ubora wa mtu binafsi na kipaji cha kuzaliwa, lakini uvumilivu wa kufanya kazi kwa bidii ili kuelewa nafasi iko wapi na jinsi ya kuunganisha kucheza," alisema Xavi kuhusu Félix, ambaye yuko kwa mkopo kutoka Atletico Madrid.

"Nimemwambia ajifurahishe, afurahie na tucheze mchezo wa kushambulia ambao unaweza kupata ubora zaidi kutoka kwa sifa zake."

# Nagelsmann kocha mpya Ujerumani

**BERLIN, Ujerumani**



JULIAN Nagelsmann anatarajiwa kutangazwa kocha mpya wa timu ya taifa ya soka ya wanaume ya Ujerumani.

Anatarajiwa kuteuliwa kwa kupewa mkataba wa muda mfupi hadi michuano ya Euro 2024, ambayo Ujerumani itakuwa mwenyeji.

Nagelsmann mwenye umri wa miaka 36 atachukua nafasi ya Hansi Flick, aliyetimuliwa Septemba 10, mwaka huu kufuatia Ujerumani kupokea kichapo cha mabao 4-1 kutoka kwa Japan katika mechi ya kirafiki ya kimataifa.

Hakuwa katika nafasi yoyote ya ukocha tangu alipoonyeshwa mlango wa kutokea Bayern Munich hapo Machi, mwaka huu.

Michuano ya Euro 2014 itaanza Juni 14, 2024 ambapo Nagelsmann atakuwa na mechi tatu za kirafiki za kimataifa kati ya sasa na michuano hiyo.

## HABARI MICHEZO

361,566/-

# MASHABIKI WANNE NAMUNGO FC WAFARIKI, TFF, KLABU ZAWALILIA

**Na Shufaa Lyimo**

MASHABIKI wanne wa Namungo FC wamefariki dunia na wengine 25 wamejeruhiwa katika ajali ya gari iliyotokea wakiwa njiani kuelekea Dar es Salaam kwa ajili ya kushuhudia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga iliyochezwa jana usiku.

Ajali hiyo ilitokea jana alfajiri katika eneo la Miteja, mkoani Lindi wakati basi la mashabiki hao lilikuwa linatokea Ruangwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Pili Mande, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kuongeza majeruhi walipelekwa katika Kituo cha Afya cha Tingi.

Mande alisema chanzo cha ajali hiyo kilitokana na dereva kuendesha kwa kasi na alipofika eneo hilo gari liliacha njia na kupinduka.

Aliongeza dereva wa gari hilo amevunjika uti wa mgongo na kwa sasa bado yupo katika Hospitali ya Sokoine na majeruhi wengine watatu ambao hali zao si nzuri wamehamishiwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Muhimbili.

Naye Mwenyekiti wa Namungo, Hassan Zidadu, alisema miili ya marehemu imerudishwa Ruangwa kwa ajili ya taratibu za mazishi.

"Ni kweli ajali hiyo imetokea alfajiri ya leo (jana) na kuhusisha mashabiki waliokuwa wanatokea Ruangwa kuelekea Dar es Salaam, kwa ajili ya kuishangilia timu yao, kwa bahati mbaya walipofika maeneo ya Miteja ndipo walipopata ajali iliyosababisha vifo vya watu wanne na majeruhi 25," alisema Zidadu.

Wakati huo huo, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Simba, Yanga na klabu mbalimbali zimetoa pole kwa Namungo kufuatia vifo vilivyosababishwa na ajali hiyo.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), wakiwasili Ivory Coast kwa ajili ya mechi ya kwanza ya kufuzu fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON 2024) dhidi ya wenyeji itakayochezwa kesho nchini humo. **PICHA: TFF**

# Prisons yawatuliza mashabiki wake

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Prisons wamewatoa hofu mashabiki wao wakisema licha ya kuanza vibaya msimu mpya, wanaamini watakaa sawa na kupata matokeo mazuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazofuata.

Akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake, straika wa timu hiyo, Batshi Mambote, alisema kwa sasa kikosi chao kimeimarika na waamini sasa hawatapoteza tena pointi.

Mambote alisema kila mechi sasa kwao ni sawa na fainali, hivyo wamejipanga kucheza kwa juhudi ili kufikia malengo na kujiondoka mkiani.

"Naamini kila kitu kitakuwa sawa, katika soka hili ni jambo la kawaida, mashabiki wetu wasiwe na wasiwasi, Prisons haitokuwa timu ya kupigania kubaki Ligi Kuu msimu huu kama ilivyokuwa msimu uliopita," alisema Mkongomani huyo.

Maafande hao wanaofundishwa na kocha mzoefu, Fred Minziro, wanaburuza katika msimamo wa Ligi Kuu wakiwa na pointi moja tu.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/09/23 | 17:00 | Middlesbrough FC vs Southampton FC | 2.65 | 3.35 | 2.47 |
| 02. 23/09/23 | 17:00 | Dundee FC vs Kilmarnock FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 03. 23/09/23 | 17:00 | Airdrieonians FC vs Raith Rovers FC | 2.43 | 3.20 | 2.55 |
| 04. 23/09/23 | 17:15 | CA Osasuna vs Sevilla FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 05. 23/09/23 | 19:30 | Burgos CF vs Elche CF | 2.80 | 3.00 | 2.60 |
| 06. 23/09/23 | 19:30 | Werder Bremen vs FC Cologne | 2.55 | 3.50 | 2.50 |
| 07. 23/09/23 | 19:45 | NEC Nijmegen vs FC Utrecht | 2.55 | 3.55 | 2.47 |
| 08. 23/09/23 | 20:00 | Casa Pia Lisbon vs Vitoria SC Guimaraes | 2.55 | 3.05 | 2.80 |
| 09. 23/09/23 | 22:00 | Stade Brest 29 vs Olympique Lyon | 2.55 | 3.50 | 2.50 |
| 10. 24/09/23 | 14:00 | FC Metz vs Strasbourg Alsace | 2.85 | 3.20 | 2.42 |
| 11. 24/09/23 | 15:30 | Ajax Amsterdam vs Feyenoord Rotterdam | 2.48 | 3.60 | 2.50 |
| 12. 24/09/23 | 17:00 | Cercle Brugge vs Union Saint-Gilloise | 2.65 | 3.40 | 2.45 |
| 13. 24/09/23 | 17:15 | Real Oviedo vs Real Valladolid | 2.75 | 2.85 | 2.70 |
| 14. 24/09/23 | 17:15 | Rayo Vallecano vs Villarreal CF | 2.55 | 3.40 | 2.55 |
| 15. 24/09/23 | 18:05 | Montpellier HSC vs Stade Rennes | 2.65 | 3.45 | 2.43 |
| 16. 24/09/23 | 21:45 | Torino FC vs AS Roma | 2.85 | 2.95 | 2.55 |
| 17. 24/09/23 | 22:00 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.65 | 3.35 | 2.47 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 21/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5121 | Cpk vs Taichung Futuro FC | 1.52 | 4.00 | 4.80 |
| 15:00 | 2509 | Hai Phong vs PSM Makassar | 2.02 | 3.58 | 3.07 |
| 15:00 | 3121 | Sabah vs Hougang United | 1.38 | 4.60 | 5.60 |
| 15:00 | 3223 | Shan United FC vs Macarthur FC | 2.60 | 3.31 | 2.42 |
| 16:00 | 3203 | Farco FC vs Coca Cola | 2.94 | 2.94 | 2.46 |
| 16:00 | 4321 | Simba vs Coastal Union | 1.18 | 5.89 | 10.40 |
| 17:00 | 2867 | Jadran Dekani vs ND Beltinci | 2.83 | 3.08 | 2.31 |
| 18:00 | 2524 | Al-Ettifaq vs AL Tai | 1.64 | 3.91 | 4.90 |
| 18:00 | 3029 | Al Taawon vs Al Raed Club | 1.65 | 3.99 | 4.72 |
| 18:00 | 5414 | Dhamk vs Al Hilal Riyadh | 11.56 | 6.73 | 1.20 |
| 19:00 | 1427 | Pyramids vs Zamalek | 1.93 | 3.39 | 3.69 |
| 19:00 | 2332 | El Ittihad Alexandria vs Ceramica Cleopatra | 2.79 | 2.99 | 2.54 |
| 19:00 | 4180 | Azam vs Singida BS FC | 1.48 | 3.72 | 5.90 |
| 19:30 | 1007 | Ihud Bnei Shfaram vs Hapoel Ramat Gan | 2.22 | 3.25 | 2.80 |
| 19:45 | 1147 | Eintracht Frankfurt vs Aberdeen | 1.14 | 8.19 | 17.40 |
| 19:45 | 1657 | HJK Helsinki vs PAOK | 3.62 | 3.47 | 2.02 |
| 19:45 | 1679 | Sheriff Tiraspol vs Roma | 6.40 | 4.10 | 1.47 |
| 19:45 | 1955 | Fenerbahce vs Nordsjalland | 1.49 | 4.21 | 5.81 |
| 19:45 | 2392 | Legia Warszawa vs Aston Villa | 5.59 | 4.20 | 1.51 |
| 19:45 | 2569 | Bayer Leverkusen vs BK Hacken | 1.14 | 7.78 | 13.96 |
| 19:45 | 2818 | Karabakh vs Molde | 2.40 | 3.35 | 2.75 |
| 19:45 | 3128 | Union Saint Gilloise vs Toulouse | 2.02 | 3.50 | 3.35 |
| 19:45 | 3181 | Servette Geneva vs Slavia Prague | 3.35 | 3.50 | 2.02 |
| 19:45 | 3626 | LASK Linz vs Liverpool | 6.89 | 4.84 | 1.37 |
| 19:45 | 3894 | Rennes vs Maccabi Haifa | 1.45 | 4.41 | 6.02 |
| 19:45 | 4516 | Panathinaikos vs Villarreal | 3.20 | 3.45 | 2.09 |
| 19:45 | 4567 | Zrinjski Mostar vs AZ Alkmaar | 4.50 | 3.65 | 1.71 |
| 19:45 | 5228 | Ferencvaros TC vs Cukaricki St | 1.24 | 5.83 | 10.05 |
| 19:45 | 5555 | Racing Genk vs Fiorentina | 2.94 | 3.44 | 2.22 |
| 19:45 | 5677 | Ludogorets Razgrad vs Spartak Trnava | 1.48 | 4.32 | 5.83 |
| 20:00 | 1549 | Hermanstadt vs Steaua Bucuresti | 3.71 | 3.29 | 1.94 |
| 21:00 | 2764 | Al Ittihad Jeddah vs Al Fateh (KSA) | 1.32 | 5.45 | 7.75 |
| 21:00 | 4765 | Al Shabab Riyadh vs AL Hazm | 1.56 | 4.07 | 5.42 |
| 22:00 | 1158 | Sturm Graz vs Sporting Lisbon | 3.61 | 3.46 | 1.95 |
| 22:00 | 1561 | FC Lugano vs Bodo Glimt | 3.01 | 3.56 | 2.14 |
| 22:00 | 2439 | Viktoria Plzen vs KF Ballkani | 1.29 | 5.22 | 8.63 |
| 22:00 | 2487 | Dinamo Zagreb vs Astana | 1.26 | 5.41 | 9.63 |
| 22:00 | 2626 | Brugge vs Besiktas | 1.89 | 3.65 | 3.60 |
| 22:00 | 2959 | Ajax vs Marseille | 2.43 | 3.45 | 2.65 |
| 22:00 | 3601 | Atalanta vs Rakow Czestochowa | 1.22 | 5.82 | 11.03 |
| 22:00 | 4394 | Slovan Bratislava vs KI Klaksvik | 1.62 | 3.91 | 4.81 |
| 22:00 | 4759 | Sparta Prague vs Aris Limassol | 1.50 | 4.29 | 5.59 |
| 22:00 | 5069 | Brighton vs AEK Athens | 1.23 | 5.75 | 10.77 |
| 22:00 | 5086 | Rangers vs Betis | 2.49 | 3.34 | 2.64 |
| 22:00 | 5127 | Maccabi Tel Aviv vs Breidablik | 1.16 | 6.96 | 12.93 |
| 22:00 | 5172 | Zorya Lugansk vs KAA Gent | 7.42 | 4.61 | 1.37 |
| 22:00 | 5343 | Olympiakos vs SC Freiburg | 2.80 | 3.30 | 2.39 |
| 22:00 | 5811 | West Ham vs Backa Topola | 1.15 | 7.01 | 15.40 |
| 23:00 | 3658 | Belgrano Cordoba vs CA Platense | 2.19 | 2.76 | 3.57 |
| 23:20 | 5013 | Cusco FC vs Atletico Grau | 1.54 | 3.84 | 4.95 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Alhamisi Septemba 21, 2023

Nipashe



Guardiola afurahia ubora wa Alvarez UKURASA 21




Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki wa Namungo, Derrick Mukombozi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana usiku. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA HAWAZUILIKI

## ●●●Yaendeleza makali yake katika kipindi cha pili na kurejea kileleni...

**Na Adam Fungamwango**

YANGA hawazuiliki! Namungo FC walijipanga kuwazuia mabingwa watetezi kupata bao wala ushindi, lakini Wanajwangani wakatumia dakika tatu za mwisho kujihakikishia kubaki kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana.

Kiungo mtokea benchi, Mudathir Yahaya alifunga bao ushindi dakika ya 87 na kuifanya timu yake kupata ushindi wa goli 1-0, ikikusanya pointi tisa na mabao 11 mpaka sasa.

Akiingia kuchukua nafasi ya Pacome Zouzoua, Mudathir aliunganisha kwa mguu wa kulia pasi ya pembeni kidogo mwa uwanja iliyopigwa na Yao Kouasi na kusababisha nderemo na vifijo kutoka kwa wanachama na mashabiki waliokuwa uwanjani hapo ambao baadhi walionekana tayari wameshakata tamaa au kuondoka.

Mpira ulionzia kwa Jesus Moloko ambaye naye aliingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Clement Mzize, akiwa kwenye wingi ya kulia, aliuingiza mpira ndani kwa Stephane Aziz Ki ambaye aliupenyeza mbele kwa pembeki kidogo mwa uwanja baada ya kumwona Yao anakimbia kwenye nafasi.

Mchezaji huyo ambaye aliwapita mabeki wa Namungo, Erasto Nyoni na Abdallah Zacharia akaukuta mpira huo na akauingiza ndani ya 18 kabla mfungaji hajaunganisha na kumpita kipa, Deogratius Munishi 'Dida' ambaye alifanya kazi kubwa sana katika mechi ya jana.

Linakuwa ni bao la pili kwa Mudathir kwenye Ligi Kuu msimu huu mpaka sasa ambapo Agosti 23, mwaka huu alifunga goli la dakika ya 75 kwa staili hiyo hiyo kwa mguu wa kulia ndani ya eneo la hatari katika mechi ambayo Yanga ilicheza dhidi ya KMC, ikishinda mabao 5-0.

Kama kawaida yake Yanga ilianza mechi kwa kasi na dakika ya kwanza tu tayari ilishapiga hodi kwenye lango la Namungo ambapo nusura ijipatie bao.

Alikuwa ni Yao aliyepiga krosi ya juu ambayo ilimpita kichwani Dida, lakini ilikosa muunganishaji huku Maxi Nzengeli akikosa bao la wazi dakika ya 20 wakati mashabiki wote wa Yanga wakiwa wamesimama, alipobaki na Dida lakini shuti lake hafifu la mguu wa kulia lilitoka nje na kushindwa kuitendea haki pasi ya Aziz Ki.

Kwa dakika 27 za mwanzo wachezaji wa Namungo walionekana kucheza kwa wasiwasi na kufanya makosa mengi na iliwachukua dakika hizo kabla ya kufanya shambulizi la kwanza langoni mwa Yanga.

Ilikuwa ni dakika ya 28 Namungo ilipofanya mashambulizi mawili mfululizo makali langoni mwa Yanga, Hashim Manyanya akipiga nje shuti kwa pasi iliyotoka kwa Jacob Massawe, na ndani ya dakika hiyo huyo kombora la mbali la mchezaji wa zamani wa Wanajangwani hao, Frank Domayo lilitoka nje kidogo ya lango na kuwaweka salama mabingwa hao watetezi.

Nafasi ya karibu na nzuri zaidi kwa Namungo kufunga bao ilikuja dakika ya 31, wachezaji wa timu hiyo walipogongeana na pasi ya mwisho ikapenyezwa kwa Massawe akiwa amebaki na kipa, Djigui Diarra, lakini alijigongagonga na kuchelewa kupiga kabla ya mabeki wa Yanga kufika na hata alipofanya hivyo uliwababatiza na kuokolewa.

Bado Yanga nayo ilifanya mashambulizi mengine mawili dakika ya 33 kupitia kwa Pacome Zouzoua alipopiga shuti la kushtukiza akiwa mbali, Dida aliufuata akauteka kabla ya kuudaka tena, na kipa huyo alifanya kazi ya ziada dakika tatu baadaye aliporuka juu kama mkizi kuudaka mpira wa Aziz Ki.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko, ambapo mbali na Moloko na Mudathir, Namungo waliwaingiza Hassan Kibailo, James Mwashinga na Zacharia, lakini walishindwa kuhimili vishindo dakika za mwisho.

# Simba yaitisha Coastal Union

**Na Saada Akida**

POINTI tatu ni muhimu, hayo ni maneno ya Simba kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union utakaochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' alisema wachezaji wake wako tayari kuelekea mchezo huo kutokana na maandalizi mazuri ambayo wamefanya.

Robertinho alisema malengo ya kikosi chake ni kusaka ushindi katika mechi hiyo na vile vile wamejipanga kuonyesha kiwango bora.

"Hatuendi uwanjani kucheza tu, tuna malengo yetu, wachezaji watakuwa makini kutumia vizuri nafasi tunazotengeneza ili kupata ushindi mnono, tunawaheshimu Coastal Union, ni timu nzuri tutacheza kwa umakini mkubwa ili kufikia kile kinachotarajiwa," alisema Robertinho.

Aliongeza baada ya mechi na Power Dynamos ya Zambia, walianza kufanya maandalizi ya mechi ya ligi mapema kwa kuwapa mbinu mpya na anaamini ataanza kuifanyia kazi katika mchezo wa leo.

Naye Kocha Msaidizi wa Coastal Union, Fikiri Elius, alisema wachezaji wake wako vizuri na wanaiheshimu Simba kwa sababu ni timu kubwa na mara zote wanapokutana wanapoteza.

Elius alisema wanacheza mchezo huo kwa tahadhari kubwa kutokana na kutambua ubora wa Simba ulipo na wanaamini wanaweza kupata matokeo mazuri na kutoka katika nafasi ya chini waliyopo sasa.

Katika hatua nyingine, Kocha Mkuu wa Azam FC, Bruno Ferry, amesema wanatarajia kukutana na ushindani katika mechi yao dhidi ya Singida Fountain Gate itakayochezwa leo usiku kutokana na wapinzani walivyoonyesha kiwango kizuri kwenye mchezo wao wa Kombe la Shirikisho Afrika.

"Maandalizi yetu yako vizuri kila sehemu ikiwamo safu ya ushambuliji ambayo ina Kagere (Meddie), Kazadi (France) na Ulimwengu (Thomas), ninaimani utakuwa mchezo mzuri na tunahitaji kupata ushindi kwa sababu ya mechi za awali za ligi hatukuwa na matokeo bora," alisema Thambo Senong, Kocha Msaidizi wa Singida Fountain Gate.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >